**Mzee** Mwinyi ampongeza Rais Samia kwa kuanza vizuri

UKURASA 5



**Mbunge** kuwasilisha muswada binafsi bungeni makato HESLB

UKURASA 5

Nipashe TESA
Jumanne Aprili 13, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Rais hataki madarasa ya chini ya miti

ELIMU

## Mradi maji Victoria utakavyoongeza ari mpya kwa wasichana kitaaluma

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

WANAFUNZI wa kike wanaosoma shule za vijijini hasa za kata, wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi katika kutimiza ndoto zao za kufanikiwa kitaaluma, mojawapo ya matatizo hayo ni kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni, uhaba wa mabweni na ukosefu wa maji safi na salama kwa wanaoishi mabwenini.

Sera ya maji ya mwaka 2002, inaeleza kuwa ifikapo mwaka 2025 asilimia 85 ya wananchi wa vijijini watapatiwa maji safi na salama



Wananchi wakifurahi maji yalipofika kijijini kwao. **PICHA: MARCO MADUHU**..

> Pia tunapofuata maji haya umbali mrefu tunachoka sana hata kushindwa kujisomea vizuri sababu ya kutembea yote hayo husababisha kushuka kitaalamu ...

Anasema wanapokuwa wakifuata huduma hiyo kijiji jirani cha Mwamatongo, hukumbana na wanaume ambao baadhi yao hujikuta wakiingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na kisha kuambulia ujauzito na kukatisha masomo kutokana na hadaa za wanaume.

"Pia tunapofuata maji haya umbali mrefu tunachoka sana hata kushindwa kujisomea vizuri sababu ya kutembea yote hayo husababisha kushuka kitaalamu tofauti na matarajio yetu ya kuendelea kuongoza kwenye mitihani na kuwashinda wavulana,"anaongeza Eta.

Aidha, anasema kuanza kwa mradi wa maji safi na salama shuleni hapo, ambao unatekelezwa na RUWASA, itakuwa mkombozi kwao kutimiza ndoto zao, sababu ya kuondokana na adha ya kusaka maji umbali mrefu.

Takwimu za mwaka 2012 zinaitaja Shinyanga kuwa inaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora asilimia 58, ya tatu ni Mara asilimia 55 yote hayo husababisha watoto kuzima ndoto zao pale wanapopewa ujauzito na kuacha masomo.

Mkuu wa Sekondari ya Masengwa, Salu Jackson, anashukuru kufikiwa na mradi huo wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria shuleni hapo, ambao utaondoa changamoto za mimba kwa wanafunzi, pamoja na kupandisha shule kitaaluma zaidi.

Anasema kutokana na ukosefu wa maji safi na salama shuleni hapo, wanafunzi wa kike ambao wanaishi bweni hukumbana na changamoto nyingi wakati wakiwa njiani kufuata maji hayo.

"Takwimu za mwaka 2020, wanafunzi wawili walipewa ujauzito, ambapo na mwaka huu wengine wawili wameshapewa ujauzito na kuacha masomo," anasema Jackson.

"Licha ya kukumbana na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama shuleni hapa, wanafunzi hawa wa kike wamekuwa wakifanya vizuri pia kitaaluma kuliko wavulana sababu ya kuishi bweni," anaongeza Mwalimu Mkuu.

Aidha, anataja matokeo ya kidato cha nne mwaka jana ya kidato cha nne shuleni hapo, kuwa ufaulu daraja wa kwanza walipata wasichana watatu tu, daraja la pili walipata wasichana 11 na wavulana tisa, daraja wa tatu walipata wasichana tisa na wavulana tisa, na daraja la nne wasichana walikuwa 32 na wavulana 11.

Aziza Joseph ni mama ambaye anaishi Kijiji cha Masengwa anasema mradi wa maji kwenye kijiji hicho, licha ya kuwa mkombozi kwa mabinti zao kuwaepusha kufuata maji umbali mrefu na kukutana na vishawishi vya wanaume wanaowapa ujauzito, utawapunguzia tatizo la kupoteza muda na kuwawezesha kufanya shughuli za kiuchumi.

Anasema mradi huo wa maji utakapokamilika ukichukua maji kutoka Ziwa Victoria, utakuwa mkombozi kwenye kijiji hicho na utawaepusha pia wanawake kuamka saa 11 alfajiri kufauta maji, kukumbana na wanyama hasa fisi na kuhatarisha maisha yao.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) mkoani Shinyanga, Juliet Payovela, anasema mradi wa maji katika Kijiji cha Masengwa ulianza kujengwa Novemba mwaka jana na unatarajiwa kukamilika na kuanza kutoa huduma ya maji kuanzia mwezi Machi.

Anasema mradi huo wa maji unaogharimu Shilingi milioni 234, umeshasambaza gata na mikingio ya kuchotea maji kijijini humo na katika Sekondari ya Masengwa ili kuwaondolea adha wanafunzi hao kufuata maji umbali mrefu na kupoteza wakati huku baadhi wakitumbukia kwenye vishawishi vinavyowaingiza kwenye majanga ya mimba za utotoni.

UKURASA 11

Jumanne Aprili 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580549

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# TRA yamjibu Mbowe

• **Yaanika** utaratibu wa kufuata wanaoilalamikia... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**MKURUGENZI ADAIWA KUTISHIWA MAISHA**
MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe...

UKURASA WA 5
**TUCTA YAJA NA KILIO CHA NYONGEZA MISHAHARA**
RAIS wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini(TUCTA), Tumaini Nyamhokya...

## DED Temeke adaiwa kuweka waandishi chini ya ulinzi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, ambaye alifika kumsalimia Rais Samia nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

## Wabunge wasema sheria ya utakatishaji inatumika vibaya

UKURASA 3

**MICHEZO** **MTIBWA HOFU KWA SIMBA KESHO** UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# TRA yafafanua malalamiko ya Mbowe

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetoa ufafanuzi wa utaratibu unaotakiwa kufuatwa kwa walipakodi wanaodai kufilisiwa fedha kwenye akaunti zao.

Pia, imesema malalamiko ya Mwenyekiti wa Chama Cha Demokrasia na Maendelo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kufilisiwa fedha zote kwenye akaunti zake za biashara na binafsi ni baina yake na TRA na sio kuzungumzia kwenye vyombo vya habari.

Juzi, Mbowe kupitia vyombo vya habari alisimulia namna Mamlaka hiyo, ilivyofilisi akaunti zake, biashara kiasi cha kukimbilia nje ya nchi kuwekeza.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alitoa ufafanuzi huo jana baada ya gazeti hili kutaka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya malalamiko ya wafanyabishara waliodai kufilisiwa na fedha kuchukuliwa kwenye akaunti zao.

Pia, wafanyabaishara wangapi akaunti zao zimefunguliwa baada ya agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

"TRA ina utaratibu wake wa ku-deal (kushughulika) na walipakodi wake, ina faili na mawasiliano ya mlipakodi mmoja mmoja, kwa hiyo inapokuwa na neno na mteja inamtafuta na mteja naye anapokuwa na neno na TRA anatakiwa aitafute kupitia njia mbalimbali zilizowekwa," alifafanua Kayombo.

"Kisheria hairuhusiwi kuweka hadharani taarifa za mlipakodi. Kwa hiyo hata Mbowe au mlipakodi yeyote anapokuwa na malalamiko yake, anatakiwa awasiliane na TRA moja kwa moja, na hatuwezi kujibu malalamiko kupitia vyombo vya habari. Kama umekutwa na jambo lolote unatakiwa uwasiliane na TRA moja kwa moja na taratibu za malalamiko zipo."

Gazeti hili awali lilimtafuta Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, ili kupata upande wake kama ameanza kushughulikia maagizo aliyopewa na Rais Samia.

"Bado sijafika ofisini na sijafungua faili lolote, watafute waliopo ofisini, ofisi haitembei na mtu," alijibu Kamishna Kidata kwa kifupi.

Kamishna Kidata aliteuliwa Aprili 4 na kuapishwa Aprili 6, mwaka huu, katika uapisho huo Rais Samia alitoa maelekezo maalum ya kumtaka kuchukua hatua ya kurejesha walipakodi ambao walilalamika kufungiwa akaunti na fedha kuchukuliwa kibabe.

"Mtamtisha (mfanyabiashara) na kumpiga kesi ya uhujumu uchumi, anaogopa kwenda jela, atajikwangua atalipa, lakini unaua biashara yake, anaifunga, kesho na keshokutwa nani atakulipa hiyo kodi."

Rais Samia alisema kinachomshangaza ni watu wanaowapigia miaka mitano au 10 nyuma anakwenda na cheti cha kulipa kodi TRA, lakini anaambiwa alikiuka hiki au kile alipe.

"Alipokiuka hiki wewe ulikuwa wapi? Kama alikiuka kwa nini ulimpa cheti cha kulipa kodi? Leo unamrudia unampiga kodi tele za nyuma aje alipe, anashindwa anafunga biashara anaogopa kwenda jela, ninaomba mkalizame hili, kodi alipe lakini kodi za dhuluma hapana, kwa sababu hazitatufikisha mbali," alionya Rais Samia.

Aliagiza wakaangalie vikosi kazi walivyoviunda na namna ya kukusanya kodi na kuwarudisha wafanyabiashara.

"Ninajua kwa uamuzi yangu tutayumba miezi mitatu au mitano tutashuka kidogo, lakini watakaporudi wakaanza kulipa tena tutapanda kwa wingi," alisema Samia.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini, Masanja Kadogosa, akimwonyesha Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mwita Waitara kuhusu hatua za ujenzi wa jengo la abiria katika stesheni ya Dar es Salaam-Morogoro wakati alipotembelea mradi wa SGR mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# DED adai kutishiwa maisha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Hanji Godigodi, amesema maisha yake yako hatarini kutokana na kutishiwa na kiongozi mmoja wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo baada ya kukataa kuidhinisha malipo ya Sh. milioni 12 ya zabuni hewa.

Taarifa za tukio hilo la kutishia kwa maneno zimefunguliwa katika kituo kikuu cha polisi Vwawa na kupewa namba MBZ/IR/200/2021.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alipoulizwa na gazeti hili alithibitisha suala kuripotiwa katika kituo cha polisi, lakini lilishughulikiwa kiutawala.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbozi, Hanji Godigodi, alipoulizwa alikiri kutishiwa maisha na kiongozi wa chama mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Katibu Tawala mkoa huo.

Alisema baada ya tukio hilo alikwenda kutoa taarifa katika kituo kikuu cha polisi Vwawa Machi 2, mwaka huu na polisi wanaendelea kuchunguza suala hilo.

Taarifa ambazo zimethibitishwa na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, zilidai mkurugenzi huyo amekuwa akitishiwa kuuawa na kigogo huyo wa CCM (jina linahifadhiwa) baada ya kukataa kuidhinisha malipo ya Sh. milioni 12 ambayo kiongozi huyo wa chama anadai kusambaza vifaa vya ujenzi ambavyo ni nondo na saruji katika halmashauri hiyo vyenye thamani hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya kutoa taarifa alipewa namba ya faili ya upelelezi (RB), lakini tangu atowe taarifa vitisho vimeendelea hali inayomfanya aishi kwa wasiwasi mkubwa.

Godigodi alisema amekataa kuidhinisha malipo hayo kwa kigogo huyo wa CCM kwasababu ameshindwa kuwasilisha nyaraka zinazoonyesha kama kweli alisambaza vifaa hivyo vya ujenzi katika halmashauri hiyo.

# DED adaiwa kuweka waandishi chini ya ulinzi wa polisi saa tatu

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI wa Manispaa ya Temeke, Lusabilo Mwakabibi, amedaiwa kuagiza kukamatwa na kushikiliwa kwa saa tatu waandishi wa habari wawili, Christopher James wa Redio One na Dickson Bilikwija wa Island TV kwa kuhudhuria mkutano wake na wafanyabiashara wa soko la Mbagala Kuu bila ya ruhusa yake.

Mkurugenzi huyo, anadaiwa kutoa amri hiyo muda mfupi baada ya kuingia kwenye kikao hicho na kukuta waandishi hao wawili waliokuwa wamepewa mwaliko na wafanyabiashara hao, akidai hawakupaswa kuhudhuria.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana mmoja wa waandishi waliokamatwa na kuwekwa chini ya kizuizi kwa amri ya mkurugenzi huyo, Billikwija, mwandishi wa wa Island TV, alisema wakiwa katika eneo hilo la kikao, Mwakabibi alihoji sababu za wao kuwapo hapo na kuagiza wawekwe chini ya ulinzi wa polisi.

"Sisi tulienda kwenye mkutano ule kwa mwaliko wa wafanyabiashara ambao walikuwa na malalamiko yako hivyo wakatuambia watakuwa na mkurugenzi hivyo tuhudhurie ili kupata taarifa kamili ya pande zote, lakini alipokuja mkurugenzi aliagiza tukamatwe na tuwekwe chini ya ulinzi kwa madai hatukupaswa kuhudhuria," alidai Bilikwija.

"Baada ya kikao kumalizika, Mwakabibi aliagiza mmoja wa watumishi wake kuwaambia askari waliokuwa wametushikilia katika moja ya makontena katika manispaa hiyo watuachie kwa onyo kuwa tusirudie tena na wakatusindikiza hadi mlangoni."

Naye James aliiambia Nipashe kuwa, walihudhuria mkutano ule ikiwa ni muendelezo wa habari waliyokuwa wakiifuatilia kuhusu malalamiko ya kikundi cha wafanyabiashara wajulikanao Super Genge Group ambao walidai mkurugenzi huyo kuwanyang'anya maeneo yao ya biashara na kuwagawia wafanyabiashara wengine.

"Kwa sababu habari ilikuwa inaendelea na Mkurugenzi hakuwa akilitolea ufafanuzi suala hili, wafanyabiashara walitualika ili tufahamu undani wake, lakini jambo la ajabu na kusikitisha mkurugenzi akatukamata bila ya kosa lolote," alilalamika James.

Bakari Lulela, mwandishi wa habari wa gazeti la Majira ambaye alifanikiwa kujibanza katikati ya wafanyabiashara bila kugunduliwa na Mkurugenzi huyo, aliiambia Nipashe kuwa baada ya mkutano kumalizika wafanyabiashara walishinikiza kuachiwa kwa waandishi hao.

Alisema baada ya sintofahamu kuendelea kuzuka, Mkurugenzi aliagiza mmoja wa maofisa kuwachukua na kuwapeleka ofisini kwake waandishi hao ambao kabla ya kuonana nao aliagiza waachiwe.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mbagala Kuu, Hamis Makeo, alikiri kuwaalika na kushuhudia tukio la udhalilishaji walilofanyiwa waandishi hao na kuwa liliwasikitisha.

Alisema waliodhulumiwa maeneo yao walikuwa wakimiliki tangu miaka ya 1980 na wamekuwa wakimsihi Mkurugenzi huyo kuwarejeshea vizimba 404 na fremu 226.

Alisema baada ya kikao hicho Manispaa ililegeza msimamo kwa kuwakubalia wafanyabiashara hao kuendelea na shughuli zao, lakini siyo kurudishiwa vizimba na fremu.

Mwakabibi alipoulizwa na Nipashe kwa njia ya simu sababu za kuwakamata na kuwaweka chini ya ulinzi wa polisi waandishi hao wa habari, alidai taarifa hizo hajazisikia.

"Ndio kwanza nimesikia kutoka kwako," alijibu Mkurugenzi huyo na kukata simu.

# Wabunge: DPP anaitumia vibaya Sheria ya Uhujumu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wameitaka serikali kuutazama upya utaratibu wa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuingia makubaliano na watuhumiwa wa makosa ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi, wakidai DPP anaitumia vibaya Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Wakati wa mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) bungeni jijini Dodoma jana, Mbunge wa Viti Maalum, Judith Kapinga, alisema Sheria ya Uhujumu Uchumi illikuja baada ya Septemba 11, ikisisitizwa kupelekwa katika nchi za Bara la Afrika ikiwamo Tanzania.

"Tulipokosea tulifuata mapokeo bila kuangalia mazingira yetu ya ndani na vilevile hatari zaidi tulipopata sheria hii, hatukuwa na uwezo wa kujadili wala kuendesha mashtaka haya na hivyo tukajikuta tunapokonya haki za watu za dhamana.

"Lakini vilevile tukapoka mali za watu kwa kudhania kuwa sheria inaruhusu. Wakati kimsingi labda ilikuwa ni tafsiri mbaya ya sheria ama sheria hazikukaa sawa ama matumizi mabaya ya nafasi pamoja na madaraka ya waliodhaminiwa," alisema.

Judith alisema hilo ni kwa sababu makosa mengi katika sheria za nchini huwa yana dhamana, akitolea mfano makosa ya wizi, ukwepaji wa kodi lakini ilivyokuja Sheria ya Uhujumu Uchumi dhamana ikanyimwa.

Alisema watafsiri wa sheria wamewafelisha katika sehemu moja ya kuwa makosa ya uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha ni matokeo ya msingi.

"Yaani leo umetuhumiwa kuiba ama ukwepaji kodi mpaka ukwepaji kodi uwe established (uthibitike) ndipo unaweza kujua ukwepaji kodi ndiyo ulisababisha utakatishaji wa fedha, ndipo hapo unapohukumiwa kwa uhujumu uchumi," alisema.

Judith alisema makosa ya utakatishaji wa fedha ni magumu kuyathibitisha lakini Ofisi ya DPP waliamua kurahisisha maisha kwa sababu ni ngumu sana kuyathibitisha.



Biswalo Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)

Alisema ofisi hiyo imeamua kwenye kosa la msingi ambalo lina dhamana, inaweka na utakatishaji wa fedha na kwa sababu halina dhamana, wanampeleka mtuhumiwa rumande.

"Hapo wanakuja na majadiliano ya bargaining, anakwambia sasa una mashtaka haya na sasa utakaa rumande miaka na miaka na kwa sababu uko 'frustrated' (umechanganyikiwa) unawaza biashara zako, unawaza familia, unawaza mume wako ama mke wako, utakosa kujadiliana ili utoke? Utajadiliana tu," alisema.

Alisema hapo ndipo watu wanapokwa mali zao kwa taratibu ambazo siyo sahihi na kwamba huo utaratibu ni unyang'anyi bila kutumia silaha.

"Haya masuala ya sheria ninaomba sana serikali yangu iangalie upya sheria. Haina tatizo ila tafsiri ya sheria ya watendaji wetu, iangalie mazingira ambayo yatalinda utu na kipato cha watu," alisema.

Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, aliunga mkono hoja ya mbunge mwenzake, akitoa ushuhuda wa gerezani Segerea alikokutana na watuhumiwa wawili wa makosa ya aina hiyo waliopelekwa mahabusu huko kutokana na kupokea muamala wa fedha kutoka mtuhumiwa wa utakatishaji wa fedha.

Alisema hakuona sababu za wanawake hao kuwekwa mahabusu kwa muda mrefu kwa kosa ambalo limefanywa na mtu mwingine.

## RIPOTI YA CAG

# Ndugai azipa jukumu maalum kamati nyeti

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20 ikiendelea kuwa gumzo nchini, Spika wa Bunge, Job Ndugai, ameagiza uchambuzi wa ripoti hiyo uwasilishwe bungeni katika mkutano wa nne badala ya mkutano wa tano.

Uchambuzi wa ripoti hizo kwa mujibu wa utaratibu uliozoeleka wa Bunge, ulikuwa unawasilishwa bungeni wakati wa mkutano wa Novemba, lakini kwa agizo hilo la Spika, sasa utafanywa Septemba.

Spika Ndugai alitoa agizo hilo jana wakati wa mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022-2025/26).

Alizitaka kamati za Bunge za Hesabu za Serikali (PAC) na Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zikae katika kipindi hiki na kuichambua ripoti hiyo kisha kumpatia taarifa.

Spika Ndugai alisema kumekuwa na upotoshaji na uzushi kupitia ripoti hiyo wakati wenye jukumu la kuchambua na kutafsiri ni Bunge kupitia kamati zake hizo.

Alisema kuwa siyo watu wengi wenye uelewa wa kuchambua taarifa za kihasibu, akitoa mfano kuwa kunaweza kukawa na ujenzi wa kituo cha afya wa Sh. milioni 500, lakini Sh. milioni 499 zikaonekana zimetumika vizuri.

Akifafanua zaidi kuhusu mfano wake huo, Spika Ndugai alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni moja ikikosa kiambatanisho fulani ni kawaida wakaguzi wanahoji fungu zima la Sh. milioni 500.

Kiongozi huyo wa Bunge alitahadharisha kuwa unaposoma mtaani, unaweza kuona Sh. milioni 500 zimeibwa, kumbe pale ni Sh. milioni moja zimekosa risiti.

Alisema kuwa mhasibu akishapata risiti ya Sh. milioni moja, anafuta hoja hiyo, lakini watu wamekuwa wanabeba dhana kwamba mamilioni yameibwa.

Alisema kamati hizo zitaanza mapema kuchambua ripoti hizo ili waangalie ratiba yao na kuwaelimisha watu kuhusiana na Ripoti ya CAG.

Baada ya kukabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 28, mwaka huu, Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20 iliwasilishwa bungeni Alhamisi ya wiki iliyopita ikiibua mijadala ya kitaifa.

# Mwanafunzi afa akiigiza watu wanavyojinyonga

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWANAFUNZI wa darasa la tatu Shule ya Msingi Ikelu,Halmashauri ya Mji Makambako mkoani Njombe, Claud Florence (9), amefariki dunia ,baada ya kujinyonga akiwa anacheza na wadogo zake.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema jana ukio hilo limetokea mwishoni mwa wiki.

Alisema mwanafunzi huyo alikwenda shambani na wazazi wake pamoja na wadogo zake watatu, na kwamba akiwa huko alianza kucheza na wadogo zake na baadae kuchukua kikoi na kuanza kujaribisha namna mtu anavyojinyonga.

Kamanda Issa alisema baada kufanya kitendo hicho katika mti pori uliopo hapo shambani, alijikuta amening'inia kwenye mti, huku wazazi wakiwa hawana taarifa yoyote wakiendelea kulima.

Alisema wazazi walipofika walifungua hicho kikoi na kumkuta mtoto wao akiwa taabani na kumpeleka hospitali na baadae kufariki dunia.

Aidha, aliwataka wazazi kuwa makini na malezi ya watoto wao kwani malezi ya watoto ni pamoja na kuangalia aina ya michezo wanayocheza katika mazingira yanayofaa.

"Watoto hawa wamecheza michezo ya kupitiliza mpaka wamejaribisha kujinyonga na mwenzao mmoja kajiua kabisa," alisema Issah.


**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**
**(Company No. 58641)**
**(Certificate of Compliance No. 1828)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT**

**(AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish bi annually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE,** we wish to make the following public disclosure of the funds received in 2020 and their expenditure, which publication covers the reporting period from **1st January, 2021 to 30th June, 2021:**

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Emergency Medicine; Central Pathology Laboratories; Leadership Capacity-Building | 570,000 |
| **Emergency Medicine Regional Amplification:** Includes Infrastructure project at Dodoma Regional Referral Hospital | 268,000 |
| **Regional Laboratories and Laboratories IT Projects; Mentorship** | 51,000 |
| **Building Livelihoods**: Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 4,451,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,802,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2020** | **7,142,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**

# Hasara mabilioni ATCL yazua jambo bungeni

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

HASARA ya mabilioni ya shilingi iliyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), imeibua mjadala mkali bungeni.

Ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Alhamisi iliyopita, inabainisha kuwa ATCL imekuwa ikitengeneza hasara kwa miaka mitano mfululizo na mwaka huo wa ukaguzi, ilitengeneza hasara ya Sh. bilioni 60.246.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kwa miaka mitano, yaani kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20, ATCL ilitengeneza hasara ya Sh. bilioni 153.542.

Akichangia bungeni jana mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee (CHADEMA), aliibua mjadala mkali alipogusia hasara hiyo.

Mdee alikumbusha kwamba tangu enzi za CAG Ludovick Utouh na Profesa Mussa Assad, serikali imekuwa ikipewa tahadhari kuhusu biashara ya usafiri wa anga, lakini haikuzingatia mapendekezo ya wataalamu hao wa ukaguzi wa hesabu za fedha.

Mdee alikumbusha kuwa wakati wa uongozi wake kwenye Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NOAT), CAG Utouh alitoa mapendekezo 15 kuepuka hasara ATCL, lakini serikali iliyapuuza.

Alisema kuwa Profesa Assad katika mwaka wake wa kwanza wa uongozi kwenye ofisi hiyo, alitoa ripoti iliyobainisha ATCL ilikuwa imetengeneza hasara kwa miaka 10 mfululizo.

Mdee alisema CAG Assad baada ya kubaini hali hiyo, alitoa mapendekezo aliyoyaita mazuri kuiepusha serikali dhidi ya hasara hiyo, lakini ikayapuuza.

"Tulizungumza hapa bungeni kuhusu haya ya hasara ya mabilioni inayotengenezwa na ATCL, lakini upande wa huku (waliko wabunge wa chama tawala) walitupinga hapa wakati tunajadili zile Sh. bilioni 500 za ununuzi wa ndege .

"Sasa CAG anasema shirika limetengeneza hasara ya Sh. bilioni 412....," Mdee alisema huku akikatishwa na wabunge wa CCM walioomba kumpa taarifa.

Miongoni mwa wabunge waliosimama kutetea uamuzi wa serikali kununua ndege mpya, ni Emmanuel Kingu, Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), aliyesema mashirika yote ya ndege duniani yamepata hasara kutokana na kuyumba kwa usafiri wa anga kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona.

"Duniani kote shirika la ndege linaanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma ili kuwezesha ukuaji wa maeneo mengine ya kiuchumi," alisema.

Mbunge wa Ukonga, Jerry Slaa, aliunga mkono hoja hiyo ya Kingu akitahadharisha kwamba: "Kama tunataka kufufua ATCL na hapohapo tunataka shirika litengeneze faida, tunapotea."

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi (CCM), alimshukia vikali Mdee kutokana na Mbunge huyo wa zamani wa Kawe kuwaita wabunge wapya kuwa ni 'njuka', akisema: "Ndege ni huduma tu za kuwezesha maeneo mengine kama utalii. Ninamuonya Mdee kwa lugha zake za kuudhi dhidi ya wabunge wapya."

Mdee pia alikumbusha kuwa katika uongozi wa Hayati Rais John Magufuli, Deni la Taifa limepaa kutoka Sh. trilioni 41 mwaka 2015 hadi Sh. trilioni 71 akirejea Ripoti ya Benki Kuu (BoT) ya Februari mwaka huu.

Ripoti ya CAG inabainisha kuwa hadi kufikia Juni 30 mwaka jana, serikali ilikuwa imenunua ndege nane kwa gharama ya Sh. trilioni1.028 katika juhudi ya kuifufua ATCL.

"Ndege hizo zinamilikiwa na Wakala wa Ndege za Serikali na ATCL huzikodisha. Pamoja na kununua ndege, kwa miaka mitano, yaani kuanzia 2015/16 hadi 2019/20, serikali imeisaidia ATCL kiasi cha Sh. bilioni 153.711 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na maendeleo.


## KUPOTEA KWA CHETI



**BARAKA KILEWO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S2652-0063** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **KOM mwaka 2011**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/BUG/RB/81844/2021**


# TABOA, Kituo cha Magufuli wavutana

**Na Maulid Mmbaga**

MVUTANO umeibuka baada ya Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) kudai hakuna ofisi za kutosheleza, huku uongozi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Dar es Salaam ukisema kuna ofisi 200 zinazotosheleza kampuni zote za mabasi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, TABOA walisema agizo la kuhamia kituoni humo hawakubaliani nalo kwasababu ndani ya kituo hakuna ofisi za kutosha zilizokamilika, huku baadhi wameshamia kwenye ofisi zilizopo.

Kwa upande wa Meneja wa Kituo cha Magufuli, Nkhama Chilosa, anasema ndani ya kituo kuna ofisi zaidi ya 200, na kwamba kuna 120 ambazo baadhi ya wamiliki wa mabasi wameshapangisha na wako tayari muda wowote kuhamia.

Aidha, alisema wanaosema hakuna ofisi wao wenyewe ndo hawajakaa vizuri kwasababu TABOA ndio waliofanya kikao na Mkurugenzi wa jiji la Dar es Salaam wakati huo, Spora Liana, na wakakubaliana kuhusiana na hilo.

"TABOA walikubaliana na Mkurugenzi wa jiji Sipora Liana kabla jiji halijavunjwa kwamba kila mmiliki alipie kiasi flani kulingana na jinsi ambavyo walikuwa wamekubaliana kwahiyo suala hilo liko wazi penngine wamiliki wengine hawakutaka tu kuomba.

"Kuna wamiliki wengine hata kituo hawakijui wanawatumia mawakala kwa hiyo wanapata taarifa kutoka kwa watu hao halafu wanazitumia hivyo hivyo bila kuzifanyia uchunguzi ili kujua undani wake," alisema.

Ofisa Habari wa TABOA, Mustafa Mwalongo, alisema ndani ya kituo hicho hakuna ofisi ambayo iko tayari na kwamba kumekuwa na mvutano kwasababu Aprili mosi, mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, alitoa agizo hilo la kuhamia humo lakini Kamanda Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam alieleza kuwa utaratibu wa kupakia uendelee kama zamani wa kupakia abiria katika ofisi zao pamoja na wa kituoni.

Kwa mujibu wa Mwalongo, kutokana na hilo hawaelewi kuwa ni nani anayetakiwa kufuatwa na suala hilo la kuhamishia ofisi zao ndani ya kituo cha Mbezi hawakuliafiki kwa madai kuwa sehemu hiyo hakuna ofisi za kutosha.

"Ndani ya kituo hakuna ofisi za kutosha na ambazo zipo tayari na hata katika kikao tulichokaa na wahusika tulizungumzia hilo suala lakini hakuna hatua iliyochukuliwa na pamoja na tamko lililotolewa na DC lakini lilikuja tamko lingine kutoka kwa Kamanda Mambosasa kwamba watu waendelee na shuhuli zao kama kawaida mpaka serikali itakapotoa tamko," alisema.


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM
MISC. CIVIL APPLICATION NO. 148 OF 2020

TOSHIBA PLANT SYSTEMS & SERVICS CORPORATION....................APPLICANT

VERSUS

VICTOR OTIENO OLAL....................1ST RESPONDENT
ZAINAB RADHID....................2ND RESPONDENT
VOLTECH PRODUCTS AND SERVICES (TANZANIA) LIMITED....................3RD RESPONDENT
KIWANGO SECURITY GUARDS (T) LIMITED....................4TH RESPONDENT
LIVING ADVENTURES COMPANY LIMITED....................5TH RESPONDENT

AND

STANDARD CHARTERED BANK TANZANIA LIMITED....................1ST NECESSARY PARTY
STANBIC BANK TANZANIA LIMITED....................2ND NECESSARY PARTY
DIAMOND TRUST BANK TANZANIA LIMITED....................3RD NECESSARY PARTY

TO:

1. Victor Otieno Olal.
P.O. Box 31441,
DAR ES SALAAM.
2. Zainab Rashid.
P.O. Box 31441,
DAR ES SALAAM.
3. The Managing Director.
Living Adventures company Limited.
DAR ES SALAAM.

SUMMONS FOR PUBLICATION

Whereas the **Applicant** has instituted an appeal against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by a pleader duly instructed and able to answer all material question relating to the appeal or who shall be accompanied by some person able to answer all such question on the **12 day of May 2021** at 11.00am. o'clock before **Hon. Registrar** to answer the suit, you must be prepared to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

Take notice that, in default of you appearance on the day before mentioned, the appeal will be heard and determined in you absence given under my hand and the seal of this court this ....16th....day of March.2021.

DEPUTY REGISTRAR
DAR ES SALAAM ZONE



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wiliaya ya MOROGORO
Kituo Cha KINGOLWIRA Mkoa MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na 07/2021
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ELIREHEMA NDOSI WA MSAMI MBEYA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ELIPOKEA ELIUFOO NDOSI
TANGAZO

(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama ya Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri Hili Endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 09 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuzileta Mahakama kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 09 Mwezi 04 mwaka 2021



## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ISMAIL IDRIS SAWA, ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.977 CGV. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/182348/2021

# TUCTA yaja na kilio cha nyongeza ya mishahara

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Shirikisho la Wafanyakazi nchini (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, amesema endapo Rais Samia Suhulu Hassan atatoa tamko lolote kuhusiana na nyongeza ya mishahara na upandaji wa madaraja kwa wafanyakazi, atakuwa amegusa kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi hao.

Pia, alisema endapo kilio hicho kitaguswa na kufanyiwa kazi, kitaongeza hali na nguvu mpya kwa wafanyakazi hao kazini.

Nyamhokya alisema kuelekea sherehe za Mei Mosi mwaka huu, wanaamini kwamba Rais Samia ndiye atakuwa mgeni rasmi na atajibu kilio chao hicho cha muda mrefu.

"Tunaamini Rais Samia ana mambo mengi anayoyatizama, lakini kwetu sisi wafanyakazi, ukituuliza jambo gani tumelimisi kwa muda mrefu ni la nyongeza ya mishahara na kupanda kwa madaraja, naamini huko anakuona hata yeye na kinachohitajika kwa wafanyakazi,"alisema Nyamhokya.

"Kwa hiyo tunamuombea sana mama awe na afya njema, aendelee kuwa anatukumbuka sisi wafanyakazi.Na ikitokea akatoa tamko lolote litakalotugusa sisi wafanyakazi siku hiyo ya sherehe zetu, kama Mungu atamjalia akiwa mgeni rasmi, nina amini wafanyakazi watakuwa na raha na amani wakisikia maslahi yao yameguswa hasa suala la nyongeza ya mishahara na upandaji wa madaraja."

# Mzee Mwinyi: Samia ameanza vizuri

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameanza vizuri majukumu yake ya kuongoza nchi na amekuwa akipokea sifa nyingi kumuhusu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Rais mstaafu Mwinyi alifika nyumbani kwa Rais Samia kumjulia hali sambamba na kumtia moyo ambapo alimhakikishia kuwa yeye na wenzake wapo tayari kutoa ushirikiano na kumsaidia wakati wowote watakapohitaji kufanya hivyo.

"Mama ameanza vizuri, ingekuwa ni nyimbo ningesema (once more) ameanza vizuri kabisa na kila mmoja ana furaha kila raia unayemsikia anasema mama ameanza vizuri, tulikuwa na Rais mzuri sana, sasa kaacha mambo ghafla kamuachia mwenzie."

"Sasa mama naye mwanadamu atakuwa na yake na vilevile kuna mambo ambayo yameanzwa na mtu mwingine ambayo watu wanayataka wanayapenda wanamshikilia mama... tunayataka haya tulieni tunayatekeleza haya sasa hilo linafurahisha," alisema Mzee Mwinyi.

Aidha, aliwataka Watanzania kumuunga mkono Rais Samia kwa kuacha balaa, ugomvi na fitina na badala yake wawe na umoja, mshikamano na kufanya juhudi za kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

# Mbunge kuwasilisha muswada binafsi bungeni makato HESLB

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Esther Matiko, amesema atawasilisha muswada binafsi bungeni ikiwa serikali haitafanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Alitangaza kusudio lake hilo bungeni jana alipochangia mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26).

Matiko alisema lengo ni kuhakikisha wanamaliza kile alichokiita uonevu katika marejesho ya mkopo unaotolewa na bodi hiyo.

"Serikali ifanye marejeo ya sheria hii ya mikopo ya elimu ya juu. Makato ya asilimia 15 ya mshahara wa mwajiriwa ni makubwa mno ukizingatia huyu mtu anakatwa makato mengine ikiwamo PAYE, bima ya afya na mengineyo.

"Hata hiyo penati ya asilimia 10 kama akishindwa kuanza kulipa mkopo baada ya miaka miwili ni tatizo. Ni sheria kandamizi. "Huu ni mkopo kwa ajili ya kusaidia watoto wa maskini na yatima. Siyo sawa na mikopo ya benki. Ni kumdidimiza zaidi mtoto wa maskini badala ya kumsaidia.

Pia, mwongozo huo unabainisha kuwa HESLB itakata asilimia moja ya ada ya uendeshaji kwa mwanafunzi mnufaika na kwamba mnufaika ambaye atashindwa kuanza kurejesha mkopo wake baada ya kipindi cha neema cha miaka miwili baada ya kuhitimu masomo yake, atapigwa penati ya asilimia 10 ya mkopo wake.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

Relationships beyond banking

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | Up to Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | Over 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | Up to 5000 USD a day | free | - |
| | Over 5000 USD withdrawal | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | Deposit fee | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |

DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019
MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| No | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.10% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| **3.0** | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| **4.0** | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| No | ITEM/TRANSACTION | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - Individual | USD 3.00 (USD a/c) TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |
| | - Corporate | USD 10.00 (USD a/c) TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | | TSHS |
|---|---|---|---|---|
| e) | Others | - | | - |
| **5.0** | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |
| **6.0** | **Other Charges** | | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | | |
| | - Individuals | 3 | | 5,000 |
| | - Corporate | 6 | | 12,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **7.0** | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| **8.0** | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| **9.0** | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **10.0** | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 08.04. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 08.04. 2021! |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 08.04. 2021! |

OTHER DISCLOSURES
(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 4.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **5.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 2.50% | 7.25% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 08.04. 2021! |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | Head of Finance | Signed | 0 8.04. 2021! |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 0 8.04. 2021! |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TRA ijisahihishe malalamiko haya

**JUZI** Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), aliibua madai mazito dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kumfilisi fedha zote kwenye akaunti ya biashara, binafsi na aliyokuwa akipokelea mshahara wa bunge.

Alieleza namna alivyoandikiwa barua kwenye barua pepe binafsi na siyo ya kampuni, huku wakijua yuko gerezani na kila akipandishwa mahakamani alikosa dhamana.

Alibainisha kuwa barua ya awali ilionyesha anadaiwa kodi ya Sh. bilioni 2 na kutokana na kutojitetea kwa wakati alitozwa riba na deni kufikia Sh. bilioni 2.6.

Aidha, alieleza namna ambavyo kila aina ya biashara aliyokuwa akifungua ilikamatwa, iliharibiwa na kutozwa kodi kubwa kiasi cha kuamua kuacha kila kitu na kuhamishia uwekezaji wake katika nchi za Dubai na Afrika Kusini kama watu wengine duniani.

Madai ya Mbowe yamekuja siku chache baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuitaka TRA kukusanya kodi kwa kufuata taratibu badala ya kutumia ubabe na kufikilisi watu kiasi cha kesho na keshokutwa kukosa pa kwenda kukusanya.

Mbowe ni mmoja kati ya wengi wenye maumivu hayo na huenda kuna ambao wako gerezani, au wamekimbia nchi kama Rais Samia alivyoeleza, na sasa kwa mabadiliko na mwelekeo mpya ni muhimu sana ukafanyika utaratibu wa kujenga imani na ujasiri kwa wafanyabiashara.

Ni muhimu sana TRA ikakutana na jumuiya ya wafanyabiashara kuweka mambo sawa, kwanza kuwaaminisha na kuwapa ujasiri kuwa wanaweza kuendelea na biashara zao bila kubugudhiwa.

Kilio cha wafanyabiashana na wawekezaji kama Mbowe maumivu yake siyo kwao tu bali kwa watu wa kawaida kabisa, waliokuwa wameajiriwa ambao walilazimika kwenda nyumbani na kukaa mtaani bila kazi, na yanakwenda moja kwa moja kwa watoto na wategemezi wengine.

Mtu huyu hataweza kupata matibabu kwa sababu hana fedha na hana bima ya afya, mwanaye hatasoma shule nzuri aliyokuwa anasoma awali, na kama alikuwa amepanga hatalipa kodi ya nyumba na bili mbalimbali za maji, umeme na nyinginezo.

Hali hiyo itaondoa mzunguko wa fedha kwa watu na hali ya maisha itakuwa ngumu sana, hii yote ikiwa ni madhara ya kumkabili mfanyabiashara mkubwa na kukamua fedha zake.

Sasa wanawenda kuwekeza nje ya nchi, maana yake wanakwenda kuimarisha uchumi wa nchi husika, wanachangia pato la nchi husika na anaajiri watu wa nchi hiyo ambako watalipa kodi kupitia manunuzi na kodi ya mishahara.


Ajira hizi zingeenda kwa Watanzania, kipato hicho kingebaki nchini, na maendeleo hayo yangebaki nchini, ndiyo maana tunasema TRA ina nafasi kubwa sana ya kuwarudisha kupitia imani na kuwatengenezea mazingira rafiki.

Ni muhimu wafanyabishara hao wakaelezwa fedha zilizochukuliwa kwenye akaunti zao zimekwenda wapi, kama zililipia kodi za nyuma je, walipewa nafasi ya kupitia hayo madai kama ni kweli? Kama haikufanyika hivyo ni muhimu utaratibu ukafanyika kuhakikisha haki inapatikana.

Tunatarajia kuona mazingira mazuri yanarejea na elimu kwa mlipamkodi inaongezeka ili kila mmoja afurahie kulipa kodi kwa kuwa ana uhakika inakwenda kutekeleza shughuli za maendeleo.

Ni muhimu yaliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), yanafanyiwa kazi ili kuongeza morali wa kazi na kulipa kodi, kwa kuwa wananchi wanaposikia mtu amechota mabilioni na bado ameachwa akitamba mtaani, basi kila mtu ataona ni sawa kufanya hivyo, na matokeo yake ujanja ujanja utaongezeka na kuua motisha ya watu kulipa kodi kwa hiyari na kwa wakati mwafaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hakuna mbadala chakula cha mchana shuleni



Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya wanafunzi nchini, hutembea umbali mrefu kufuata elimu, huku wakishinda njaa mchana kutwa, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wazazi na walezi kushindwa kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao.

Katika hali hiyo wapo wazazi na walezi ambao hawana uwezo kifedha kwa ajili ya kuchangia mlo shuleni na hawawezi kuwapa watoto fedha za kujikimu wawapo shuleni.

Hawa ni wale ambao hata ratiba ya mlo wa nyumbani ina changamoto kwani wanaweza kula mara moja, hasa jioni, hivyo si rahisi kuchangia gharama za chakula shule au kuwapa watoto wao fedha za kununua chakula.

Lakini, pamoja na hayo, suala la chakula shuleni ni la muhimu, ingawa pia wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawataki kuchangia wakidai kwamba serikali ilishatangaza kutoa elimu bure.

Kimsingi ni kwamba, kukosekana chakula cha uhakika cha mchana shuleni kwa shule nyingi nchini ni mateso kwa baadhi ya wanafunzi na hali hiyo inaweza kuwaathiri katika kujifunza na kupata elimu bora.

Wanaotembea umbali wa kilometa tano kufuata au zaidi ya hapo kufuata elimu, halafu wanashinda njaa, hivi kweli wanaweza kusoma vizuri kama siyo mateso hayo?

Serikali imeweka wazi kuwa suala la michango kwa ajili ya chakula liachwe mikononi mwa wazazi na walezi bila kuhusisha walimu bali wabaki kutoa eneo la kuhifadhia chakula, hivyo ni vyema wahusika wakaona umuhimu huo.

Naibu Waziri TAMISEMI, David Silinde anatoa maelekezo hayo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Songwe kujadili baadhi ya shule kutotoa chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Katika msisitizo wa kuwapo kwa chakula shule, Ofisa Elimu Sekondari Manispaa ya Morogoro, Dk. Janeth Barongo, alisema kwamba, wazazi anatakiwa kuwa desturi ya kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao shuleni.

Anaamini kwamba, hatua hiyo inaongeza kiwango cha ufaulu, kwa kuwa watoto wengi wamekuwa wakifeli kutokana na utoro ambao unasababishwa na ukosefu wa chakula shuleni.

Ni mwaka jana, Dk. Barongo, anasema hayo katika ziara ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro na kufafanua kuwa tatizo linalozikumba shule nyingi kutokuwa na chakula shuleni, ni kwa sababu ya wazazi kutochangia fedha.

Binafsi ninadhani kwamba, umefika wakati sasa wazazi na walezi kuwa na mwamko wa kuchangia chakula shuleni, kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao kielimu badala ya kujiweka pembeni.

Njia za kuchangia zipo nyingi, mzazi au mlezi ambaye hana fedha, bado ana nafasi ya kuchangia chakula kuliko kukaa kimya na kuacha watoto wakitembea umbali mrefu kuafuta elimu, huku wakishinda njaa.

Suala la ushirikiano kwa ajili ya elimu ya watoto wao kwa kuchangia fedha na chakula halikwepeki, hasa kwa kuzingatia kwamba, serikali inatoa elimu bure, hivyo ingekuwa vyema wazazi na walezi wakafanya sehemu yao.

Mbali na kusaidia wanafunzi kusoma vizuri, kuwapo kwa chakula shuleni kunaweza pia kupunguza utoro kwa wanafunzi, kwa kuwa kuna uwezekano baadhi yao kutohudhuria shule kwa kuhofia kushinda njaa.

Kwa ujumla, wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kufuata elimu bila kula, inawawia vigumu kuwa na usikivu darasani, hivyo ni vyema wadau wakatafakari na kuchukua hatua kuchangia upatikanaji wa chakula shuleni.

Zipo baadhi ya wilaya na mikoa familia zimekuwa zikichangia fedha na chakula kwa ajili ya watoto wao kwa lengo la kuhakikisha wanawaowandolea usumbufu na kuongeza ufaulu.

Utaratibu huo ungefaa kuigwa nchini kote ili kumaliza tatizo hilo la kuwaacha watoto kushinda njaa shuleni wakati uwezekano wa wazazi na walezi kutoa mahindi, maharage, mboga au mchele ili kuwapa chakula upo.

Hivyo siyo kuchangia chakula bali pia linapokuja suala la uhaba wa madarasa na madawati, wazazi na walezi bado wana nafasi ya kuchangia wa miundombinu hiyo ya shule badala ya kusubiri kila kitu kifanywe na serikali.

Kudhani kwamba, jukumu la kusimamia elimu kwa watoto wao ni la serikali peke yake, pengine siyo sahihi kwani familia zina sehemu ya kufanya kwa ajili ya kuboresha elimu ya watoto wa taifa hili.

# TPSF yakoshwa na Samia mwelekeo wa biashara

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Sekta Binafsi (TPSF), imepongeza hotuma iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 6, mwaka huu na kwamba imetoa mwelekeo mpya na dira katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Pia, ilisema Rais Samia ametoa dira na mwelekeo mpya katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, kukuza na kuendeleza uhusiano ya kimataifa kwenye diplomasia ya uchumi, azma ya kujenga viwanda katika kila mkoa ili kukuza uchumi na kuongeza ajira pamoja na kuwekeza kwenye kilimo biashara na kukuza uchumi wa bluu.

Ilimpongeza kwa kuiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kukusanya kodi kwa weledi na kutokutumia mabavu ili kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula, alisema miongozo na maelekezo mbalimbali aliyoyatoa Rais Samia ikiwamo kutaka kuitishwa kwa mikutano ya kisekta yanaonyesha nia njema ya kulenga kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza ushiriki mpana wa shughuli za kujenga uchumi.

"Katika hotuba, Rais alishauri na kuelekeza namna bora ya ukusanyaji wa mapato. Sekta binafsi tunampongeza kwa hatua hii kwani imekuwa ni changamoto ya muda mrefu,"alisema Ngalula.

"Hotuba ya Rais ya Aprili 6, mwaka huu, imefungua ukurasa na kuleta matumaini mapya.Mheshimiwa Rais ni deni kubwa kwa sekta binafsi na tutalilipa kwa kuhakikisha tunasimama katika misingi ya uzalendo na uadilifu katika suala la ulipaji kodi ili kazi iendelee kwa kasi zaidi."

"TPSF inaunga mkono maagizo yote ya Rais Samia na tutashirikiana na serikali katika hatua zote za utekelezaji wake."

TPSF pia ilishauri baadhi ya mambo ambayo serikali inapaswa kuyafanyia kazi kwa haraka kuwa ni pamoja na kuhakikisha inabadilisha na kuboresha mifumo ya kodi, kupanua wigo wa walipakodi ikiwamo kurasimisha biashara ambazo hazijawa rasmi mpaka sasa.

Mambo mengine iliyoshauri yafanyiwe kazi ni pamoja na kutengeneza bidhaa na huduma mpya ili kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi hususani kupitia sekta ya kilimo, kuhakikisha mazingira mazuri ya kusadia wananchi kushiriki katika uwekezaji na upatikanaji wa mitaji.

Pia iliomba serikali kufanyia kazi mapendekezo na mawasiliano mbalimbali ya kisekta ambayo taasisi ya sekta binafsi imeyatoa yenye lengo la kuboresha na kupanua wigo wa ukusanyaji mapato, kuvutia uwekezaji na kuongeza ajira.

## Malighafi yasababisha kiwanda kusimama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIWANDA cha uzalishaji mafuta ya kupikia cha Jielong kilichopo Manispaa ya Shinyanga, kimesimamisha uzalishaji baada ya kukosa malighafi.

Kaimu Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Zhongjun Ji alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea kiwandani hapo ili kuona hali ya uzalishaji wa mafuta ya kupikia.

Ji alisema kuwa kwa sasa hawafanyi shughuli za uzalishaji wa mafuta hayo ya kupikia kutokana na kukosekana kwa malighafi ya mbegu za zao la pamba.

"Uzalishaji wa mafuta ya kupikia kwenye kiwanda hiki hatufanyi tena hadi pale tutakapoanza kupata tena malighafi ambazo ni mbegu za pamba," alisema Ji.

Alisema pia wana mpango wa kuanza kuzalisha mafuta ya mawese yatokanayo na zao la mchikichi na kwamba watakuwa wakiagiza malighafi hiyo kutoka wilayani Kyela mkoani Mbeya na Ifakara mkoani Morogoro.

Katika hatua nyingine alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassani kwa hotuba yake ambayo aliitoa hivi karibuni wakati wakiwaapisha makatibu wakuu na manaibu kutoka wizara mbalimbali kuwa imewapa matumaini wawekezaji hasa kwenye ulipaji kodi kwa njia rafiki.

## Uelewa mdogo wakwamisha watu kupima afya

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, amesema uelewa mdogo kwa jamii unachangia kukwamisha watu kujitokeza kupima afya zao kubaini magonjwa nyemelezi au yasiyoambukizwa ili kuyatibu mapema.

Macha aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa mpango wa upimaji afya ili kubaini magonjwa yasiyoambukizwa kwa watumishi wa benki ya CRDB kanda ya Magharibi iliyojumuisha mikoa ya Geita, Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Alisema hivi sasa magonjwa yanayosumbua jamii ni figo na moyo, lakini bado baadhi ya watu hawana uelewa wa upimaji wa afya zao kubaini mapema magonjwa yasiyoambukizwa au nyemelezi na kupatiwa matibabu.

Meneja wa ustawi wa afya ya wafanyakazi na uwekezaji wa benki hiyo, Crescensia Kajiru, alisema mpango wa upimaji afya kwa watumishi wa CRDB ni endelevu, ili waweze kufanya kazi wakiwa na afya nzuri na kufahamu magonjwa yasiyoambukizwa.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

**PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES**

**PURSUANT TO REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019 AND REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014.**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | |
| a) Monthly | FREE | FREE |
| b) Interm | 5,000.00 | $5 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | FREE | Upto 5000 Free<br>Above 5000 - 0.3% |
| 5. Cash Deposit Charges | FREE | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | 15,000.00 | $7 |
| 7. A/c Closure charges | 15,000.00 | $15 |
| 8. Activation of Dormat A/c | 6,000.00 | $6 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | FREE | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | FREE | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly b) Interm | **5000**<br>**5000+500 for each page** | **$5**<br>**$ 5+1 for each page** |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MIO- FREE<br>ABOVE 25 MIO--0.12% | Upto 5000 Free<br>5000 to 10,000 - 0.3%<br>Above 10,000 - 0.5% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO- FREE<br>ABOVE 50 MIO--0.12% | **Upto 10,000- Free**<br>**> 10,000- 0.3%** |
| 5. Balance Confirmation certificate | 25,000.00 | $15 |
| 6. Stop Payment Charges | 30,000.00 | $15 |
| 7. Cheque Return Charges | | |
| a) Inward | 30,000.00 | $15 |
| b) Outward | 30,000.00 | $20 |
| 8. A/c closure charges | 25,000.00 | $20 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | |
| 1. Cash Withdrawal | | |
| Upto 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | |
| Upto 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | 10,000.00 | NA |
| **Mobile Banking Services** | | |
| A) Monthly Subscription Charges | 500.00 | NA |
| B) PIN Request | 2,500.00 | NA |
| **H. LOCKERS RENT YEARLY** | | |
| 1.SMALL | 350,000.00 | |
| 2. MEDIUM | 600,000.00 | |
| 3. BIG | 750,000.00 | |

| **D. REMITTANCES** | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 to 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 to 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 and above | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Upto 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $60 |
| above 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Upto 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 to 10,000 | NA | $18 |
| above 10,000 | NA | $30 |
| **E. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - 25,000 5Mio to 10 Mio - 200,000 10 Mio to 25mio - 400,000 25 mn to 500 mio - 1.5% >500mio--1.25%* *minimum 7.5mio | Upto 5,000 - $100<br>5000 to 10,000 - $200<br>Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.5%<br>>500,000--1.25%*<br>*minimum 7,500 |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 mio --NIL--<br>>100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Upto 50,000 --NIL--<br>>50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - 25,000 5 Mio to 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Upto 20,000 - $300<br>20,000 to 500,000 - 1.8%<br>>500,000--1.5%*<br>*minimum 9000 |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Upto 50,000 - 25<br>>50,000 ----50 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS 120,000 | USD 50 |
| 6.Pre-payment penalty | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Min $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Min $50 max 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Min $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Min$75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Min $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Min $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Min TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% per quarter (Min TZS 75,000) | 40% of actual charges |

**OTHER DISCLOSURES**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |
| c. Fixed deposits | | |

i. Fixed Deposits of TZS

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million up to 100 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

ii. Fixed Deposits of USD

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 up to USD 100,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| NAME | TITTLE | SIGNATURE | DATE |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 12-APRIL-2021 |
| JOHNVIAN NYAMSISA | GM-TREASURY | SIGNED | 12-APRIL-2021 |
| VICTORY NAHUM | CREDIT MANAGER | SIGNED | 12-APRIL-2021 |

# Ajali treni ya mizigo yakwamisha abiria

**Na Deogratius Nsokolo, KIGOMA**

ZAIDI ya abiria 800 wa treni ya haraka iliyokuwa ikitoka Dar es Salaam kwenda Kigoma wamekwama kwa zaidi ya saa nane baada ya treni waliyokuwa na wasafiri hao kushindwa kufika mjini Kigoma kutokana na ajali ya treni ya mizigo.

Mkuu wa kituo cha reli Kigoma, Ally Shamte, alisema treni ya mizigo ilipata ajali kati ya stesheni ya reli Kazuramimba na Kigoma, hivyo kuharibu reli.

"Tumelazimika treni iishie Kazuramimba na abiria tumewababe kwa mabasi kutoka Kazuramimba mpaka mjini na abiria waliokuwa wanasafiri nao tumewapaleka Kazuramimba kwa mabasi ili wakaanzie huko safari," alisema Shamte.

Hata hivyo, alisema jitihada zinaendelea kuhakikisha njia ya treni inatengenezwa na kukamilika kwa haraka ili safari ziendelee

Alisema mafundi wako kwenye eneo la tukio walikuwa wakiendelea na kazi usiku na mchana.

Baadhi ya abiria wamelalamika hali ya uendeshaji wa shirika hilo kutokana na kutotoa taarifa kwa wakati kwa abiria na kusababisha usumbufu mkubwa na kuongezeka kwa gharama.

Anton Cosmas, alisema usafiri wa treni hauna uhakika, wakati ndio unaotegemewa na wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

# Kunenge azionya taasisi zinazotumia dini vibaya

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, ametoa wito kwa taasisi zilizopewa usajili kwa lengo la kusaidia jamii hususani yatima na wasiojiweza kutenda haki kwa walengwa.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati alipokuwa akihutubia kongamano la mashindano ya sita ya usomaji wa Quran yaliyoandaliwa na Taasisi ya Faraja Islamic Foundation (FIF) na kusema kuna baadhi ya taasisi zilizosajiliwa kwa dhumuni la kusaidia wasiojiweza, lakini hawafanyi hivyo.

Alisema wakati mwingine anapata wasiwasi anapoalikwa na taasisi kwasababu kunachangamoto baadhi yao sio waadilifu pamoja na kuwa ni taasisi za kidini.

"Nimelisema hilo kwa sababu tunapokuwa katika taasisi za kidini tuna wajibu wa kuonesha mfano kwani unapokuwa katika sehemu hizo halafu kunakuwa na sintofahamu na sisi ndio tunaosimamia maeneo hayo inakuwa na changamoto kubwa zidi kwetu."

"Kwa hali hiyo hata yanapokuja masuala ya uhitaji wa kusaidiana wakati mwingine yanakuwa magumu kwa sababu ya hali zetu sisi wenyewe ndani ya taasisi husika kwahiyo watu ambao wanaweza kusaidia wanakaa pembeni," alisema Kunenge.

Alisema hali hiyo inajitokeza unapokuwa ndani ya taasisi na inafanya mambo ambayo hayampendezi Mungu pamoja na jamii na kwamba hakuna atakayetaka kuwa sehemu ya taasisi inayokula mali za yatima.

Pia, alisema hakuna mtu atakayetaka kuwa sehemu ya taasisi inayotumia mali za watu kwa maslahi binafsi, inayoomba misaada na kuitumia kinyume na taratibu kwasababu inamkosea Mungu na inatoa picha mbaya kwa jamii.

"Tukiwa na taasisi nzuri ambazo 'zimenyooka' mimi naamini ni rahisi kuweza kusaidiana nazo kwani tunapopata mialiko kama hii ni lazima ujiulize kuwa ni nani huyo na ufanye uchunguzi kidogo ukisha jiridhisha ndo uitikie wito."

"Hivyo ndugu zangu hilo ni suala ambalo tunatakiwa tujitathimini kwamba tunafanya mambo ya kheri, tunafanya vizuri tunashiriki kutoa misaada kwa jamii naamini tutapata watu wa kutusaidia na jinsi nilivyoona hapa naahidi tutaweza kushirikiana," alisema Kunenge.

Aliwapongeza viongozi wa dini wanaoendelea kuwafundisha watoto kusoma na kuielewa dini kwa kuwa ndani yake kuna miongozo ya maisha ya mwanadamu ni namna gani anatakiwa kuishi na mambo gani yanatakiwa kutenda na yapi hayatakiwi.

Alisema mashindano hayo yanasaidia jamii kuelewa kwa undani vitabu vya dini jambo ambalo linajenga jamii yenye maadili na hofu ya Mungu na alitoa wito kwa wanaovitumia vibaya vitabu vya Mungu kuacha tabia hiyo kwa kuwa wanatapeli watu.

"Wanaoitumia dini kwa maslahi yao wataenda kesho kujibu kwa Mungu kwani viongozi wetu wa dini tutawapa picha ambayo siyo tunaichafua dini na nimelisema hilo kama ndugu yenu silisemi kama mkuu wa mkoa tuitumie dini vizuri," alisema.

Aliipongeza taasisi ya FIF chini ya mkurugenzi wake Hashim Madenge kwa kuona umuhimu wa kuandaa mashindano ya kuhifadhi Quran takatifu na kuahidi kuwa serikali itampatia ushirikiano kwasababu anachokifanya kina manufaa kwa jamii.



Aliyekuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdalla Ulega akimkabidhi tuzo ya Mkuu wa Kitengo cha Mikakati Benki ya CRDB, Jessica Nyachiro katika tamasha la kutambua mchango wa wanawake katika jamii lililoandaliwa na kampuni ya Mwananchi Communication Ltd (MCL) mapema mwezi Machi. Wengine pichani ni, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wakwanza kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa MCL, Bakari Machumu, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Benki ya CRDB, Yolanda Urio, Mkurugenzi wa Ukaguzi Benki ya CRDB, Godfrey Sigala na Meneja Ustawi, Ujumuishi na Uwezeshaji Benki ya CRDB, Crescensia Kajiru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yafanikisha kuandaa wanawake uongozi wa juu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imewainua wanawake kiongozi na kuwawezesha kushika nyadhifa za juu za uongozi ili kuleta usawa wa kijinsia.

Moja ya hatua zilizochukuliwa ni mradi wa 'SHE Initiative' wenye kauli mbiu ya 'Redefining HER story' ulioanza kutekelezwa tangu Oktoba 2019.

" Mradi wa SHE Initiative uliwajengea uwezo wa kuwa viongozi watumishi wanawake wa CRDB Bank ili kuwa na ushiriki unaozingatia usawa wa kijinsia kwenye ngazi za juu za maamuzi."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa CRDB Abdulmajid Nsekela, aliyekuwa akizungumza jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kuelezea mafanikio ya kiuongozi yaliyofikiwa na wanawake wa benki hiyo kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema mwezi uliopita katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa CRDB, Tully Mwambapa, alitajwa kuwa 'Super Woman' kwenye sekta ya fedha.

Ni katika hafla iliyoandaliwa na taasisi ya habari kwa kushirikiana na wadau ikiwamo Women in Leadership Institute kutoka Dar es Salaam.

Nsekela alimpongeza Mwambapa, akisema ni zao la mikakati ya CRDB ya kuwawezesha wanawake kiuongozi ukiwamo 'SHE Initiative.'

"Lengo mahususi la mpango huu ni kuandaa nguvu kazi ya wanawake wenye ujuzi wa kuitumikia benki , pia kutoa ufumbuzi wa masuala ya kifedha yanayowakabili kinamama wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) hadi wakubwa na kushirikiana na kusaidia jamii kupata mafanikio na ustawi kwenye shughuli za kufanikisha miradi ya, kiuchumi, kijamii na kimazingira," alisema.

Nsekela alisema kwa miaka miwili CRDB imeanza kupata mafanikio makubwa kwenye mradi wa "SHE Program", ikiwa ni pamoja na kuwa na kongamano la wanawake wafanyabiashara uliokuwa na lengo la kuboresha uwezo wao kufedha.

Alieleza kuwa katika kongamano hilo wanawake 320 kutoka Kanda ya Ziwa walinufaika na mafunzo ya umahiri na weledi kwenye masuala ya fedha na uendeshaji miradi.

"Kupitia akaunti ya Malkia , benki imetoa mikopo ya zaidi ya Sh.bilioni 500 kwa wajasiriamali wanawake 25,000 kutoka mikoa mbalimbali, " Nsekela alisema.

Aidha, benki imewafikia wanawake kwa njia mbalimbali ikiwamo kuwapatia wasichana 5,372 taulo za kike ili kuondoa changamoto za kukosa masomo wakati wa hedhi.

HABARI KITAIFA

# Wavamizi hifadhi kuondolewa

**Na Augusta Njoji**

SERIKALI imesema haitasita kuwaondoa wananchi watakaovamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uhifadhi.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alitoa kauli hiyo alipofanya ziara katika eneo la Isawima wilayani Kaliua mkoani Tabora na kushuhudia baadhi ya wananchi katika wilaya hiyo wamevamia eneo lililohifadhiwa la Msitu wa Isawima na kuendesha shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo na ufugaji kinyume cha sheria.

Alisema yapo maeneo ambayo yalikuwa yametengwa na Serikali kwa ajili ya hifadhi, lakini kutokana na ufinyu wa maeneo wananchi wameyavamia jambo ambalo halikubaliki kwa kuwa Serikali inayatambua maeneo hayo.

Aliwataka wananchi wayalinde na kuyatunza ili yaendelee kuwapo kwa kuwa yana faida kubwa kwa kuwa ni chanzo cha mvua na maji katika maeneo yao na pia huvutia wawekezaji ambao husaidia kuongeza Pato la Taifa na kuchangia wananchi kupata huduma mbalimbali za kijamii .

"Tunahifadhi kwa ajili ya kulinda nyazo vya maji, lakini tunatarajia kuweka wawekezaji ambao watasaidia kuongeza Pato la Serikali, hili ndilo ambalo linakuja kukujengea wewe vituo vya Afya, huduma za shule kama ambavyo mnaona sasa watoto wote wanasoma elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne ,shida mliyonayo hapa ni wapi mkafanye shughuli za kilimo na ufugaji lakini maeneo ambayo bado yapo ni mengi sana," alisema.

Aliwataka viongozi wa Mkoa wa Tabora na wilaya ya Kaliua kuwajibika kuwaonesha wananchi hao maeneo ambayo siyo ya hifadhi ili kuendesha shughuli zao zikiwamo za kilimo na ufugaji.

Masanja aliwataka wananchi ambao walivamia maeneo ya hifadhi na kulima mazao ya chakula wayatoe kwa utaratibu wa vibali.

Mbunge wa Kaliua, Dk.Aloyce Kwezi, alisema maelekezo yote ambayo Naibu Waziri ameyatoa watayatekeleza kuhakikisha kuwa wanaepuka migogoro ya mara kwa mara.

**Maelekezo yote ambayo Naibu Waziri ameyatoa watayatekeleza kuhakikisha kuwa wanaepuka migogoro ya mara kwa mara.**

# Wakulima wapewa siri ya kuepuka sumu kuvu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAKULIMA wa mazao ya chakula wametakiwa kuhakikisha wanakausha mazao yao katika kiwango kinachotakiwa, ili kuepuka uzalishwaji wa sumu kuvu, ambayo ni hatari kwa maisha ya binadamu.

Akiwasilisha mada katika mafunzo ya waandishi wa habari juu ya kudhibiti sumu kuvu katika mazao, Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Dk. Happy Magoha, alisema ni vyema wakulima wakashirikiana na wataalamu wa kilimo, ili kujua upandaji bora wa mazao na kanuni za kilimo.

Alisema ili mazao yabaki kuwa salama, inatakiwa kupimwa kiasi cha unyevu kabla ya kuhifadhiwa na kuhakikisha wanayahifadhi vizuri ili kuepuka uzalishwaji wa sumu kuvu.

**Sumu kuvu ni sumu inayozalishwa na kuvu (fangasi), hivyo inaweza kupatikana katika mlolongo mzima wa chakula kuanzia kwenye kupanda, kuvuna, kukausha na kuhifadhi.**

"Sumu kuvu ni sumu inayozalishwa na kuvu (fangasi), hivyo inaweza kupatikana katika mlolongo mzima wa chakula kuanzia kwenye kupanda, kuvuna, kukausha na kuhifadhi," alisema mhadhiri huyo.

Aidha alisema kuwa, hali ya hewa katika nchi ndio inayosababisha kuvu ambayo hupelekea sumu kuvu, hivyo ni vyema kwa wakulima wakazingatia hali hewa wanapolima, ili wavune kipindi cha jua ambapo itasaidia mazao yao kukauka vizuri.

Meneja mradi wa kudhibiti sumu kuvu (TANIPAC) kwa upande wa Zanzibar, Mwanaidi Ali Khatib, alisema, lengo la mradi huo ni kupunguza utokeaji wa sumu kuvu katika vyakula, kuongeza maarifa na uwelewa kwa jamii kuhusu madhara ya kiafya na athari zake na kukuza ushirika wa sekta binafsi katika kudhibiti.

Nae Dk. Faki Ame Kessi kutoka Idara ya Mifugo Zanzibar, alisema sumu kuvu ni hatari kwa maisha ya binadamu, hivyo ni vyema kwa waandishi wa habari wakashirikiana pamoja kutoa elimu kwa jamii.

Akitoa shukrani kwa niaba ya waandishi wenzake, Haji Nassor Mohamed kutoka gazeti la Zanzibar Leo Pemba, alisema watajitahidi kutoa elimu kwa jamii kuhakikisha wanaielewa sumu kuvu na namna ya kuidhibiti katika mazao.



Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kushoto), akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Wilaya ya Kaliua wakisikiliza kero za Wananchi wa Kijiji cha Isawima mapema mkoani Tabora. **PICHA: AUGUSTA NJONJI**

# 360 kunufaika CHF iliyoboreshwa bure

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WILAYA ya Kahama imemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, kuweka watumishi maalumu katika lango kuu la kuingia hospitali ya wilaya watakaokuwa na jukumu la kuwasaidia wazee wanaofika kupata matibabu.

Anamringi Macha, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, aliyabainisha hayo wakati wa hafla ya kupokea na kukabidhi kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kwa wazee 60 sawa na wategemezi wao 360 kutoka vijiji vinne vya Kata ya Mwendakulima zilizotolewa na mdau wa afya Said Salum (Azan Logistics).

Alisema watumishi hao watakuwa wamevalia mavazi maalum ambayo yatakuwa na maandishi yasemayo "Niulize nikusaidie"na jukumu lao kubwa litakuwa kuwasaidia wazee wasipate usumbufu wanapofika hospitali ya wilaya kupata matibabu.

Macha alisema Ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wazee kukosa usaidizi wanapokwenda hospitali hiyo kutafuta matibabu, hali ambayo imekuwa ikisababisha wengi wao kushindwa kupata huduma za afya kutokana na uwapo wa idadi kubwa ya wagonjwa.

"Hospitali yetu inahudumia wagonjwa kwa siku 1,000 mpaka 1,200 kutoka maeneo tofauti, tusipoangalia namna nzuri ya kuwasaidia wazee wetu watakuwa wanakosa muda wa kuonana na madaktari au kukosa kabisa matibabu," alisema Macha.

Hata hivyo, alisema imetengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wazee kwa kuanzisha madirisha ya wazee katika wospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati na kuwataka watumishi wa sekta ya afya kuhakikisha wanawasikiliza ili kuondoa tatizo hilo.

Nae Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Lucas Ngamtwa, ambaye alimwakilisha mkurugenzi Msumba alisema watalitekeleza agizo hilo ili kuwawezesha wazee kupata huduma bora za matibabu.

# Utekelezaji mradi bomba la mafuta kuanza mwezi huu




Habari na Augusta Njoji

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliambia bunge kuwa utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga utaanza mwezi huu kwa kipindi cha miaka mitatu.

Dk. Kalemani aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akiongezea majibu katika swali la Mbunge wa Kiteto (CCM), Edward Olelekaita.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira za upendeleo kwa vijana na fursa nyingine za kibiashara kwa wananchi wa Jimbo la Kiteto kupitia mradi mkubwa ambao unapita Wilaya ya Kiteto.

Katika Majibu ya Waziri Kalemani, alisema juzi alishiriki pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan katika utiaji wa saini wa utekelezaji wa mradi huo.

"Mradi huu ni mkubwa na utapita katika mikoa nane wilaya 24, vijiji 127, vitongoji 502, mradi utatoa ajira zaidi ya 10,000 katika hatua za awali, na hadi Watanzania 15,000 katika shughuli za ujenzi na shughuli za kawaida," alisema.

**Kutokana na Bomba hilo kupita katika Wilaya ya Kiteto, wananchi wa Kiteto wanufaika na ujenzi wa mradi huo kwa kufanya biashara, ajira na fursa za kiuchumi na kijamii.**

Aliwaomba wananchi kwenye maeneo ambayo mradi utapita wajitokeze kuchangamkia hizo fursa kwa kuwa zimewekwa rasmi kwa ajili ya Watanzania.

Hata hivyo, alisema wizara yake itafanya ziara wilaya kwa wilaya ili kuhamasisha Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ikiwamo Wilaya ya Kiteto.

Awali, Naibu Waziri Stephen Byabato, akijibu swali hilo, alisema Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda, inatekeleza mradi wa ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Kabaale/Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Mkoani Tanga nchini Tanzania.

"Kwa upande wa Tanzania Bomba litapita katika Mikoa 8 na Wilaya 24 ambapo Wilaya ya Kiteto itapitiwa na bomba kwa urefu wa kilomita 117.1 pamoja na ujenzi wa kambi ya kuhifadhi mabomba katika kijiji cha Ndaleta na kambi ya wafanyakazi katika Kijiji cha Njoro,"alisema.

Alisema kutokana na Bomba hilo kupita katika Wilaya ya Kiteto, wananchi wa Kiteto wanufaika na ujenzi wa mradi huo kwa kufanya biashara, ajira na fursa za kiuchumi na kijamii.

"Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutoa hamasa ili wananchi wanufaike na shughuli za ujenzi na uendeshaji wa mradi,"alisema.



Mbunge Viti Maalum, Agnes Hokororo, akiuliza swali la nyongeza Bungeni Jijini Dodoma jana, kuhusu tatizo la maji kwenye maeneo mbalimbali nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## 'Kero za mfumo wa soko zashughulikiwa'

SERIKALI imesema inaendelea kushughulikia kero zilizojitokeza katika mfumo wa Soko la Bidhaa (TMX), kwenye maeneo yaliyofanyiwa majaribio, ili mfumo huo utumike maeneo yote yanayozalisha korosho.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibiti (CCM), Twaha Mpembenwe.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itahakikisha minada ya zao la korosho na ufuta inafanyika muda unaolingana ili kuondoa mporomoko wa bei kwa baadhi ya maeneo yanayolingana kwa misimu sawa ya kuvuna mazao hayo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashe alisema kwasasa timu ya wataalam wa wizara hiyo ipo Mkoa wa Pwani ikifanya tathmini mbili ya tatizo la ubora wa korosho ya Pwani kukosa soko tofauti na korosho ya Tandahimba.

Alisema tatizo jingine ni kutokana na mkoa huo kupata mvua nyingi kwa mwaka kuliko maeneo mengine, wakulima wa eneo hilo wamekuwa na tatizo la korosho yao kuwa na unyevu.

"Wizara ya Kilimo imeiagiza Bodi ya Korosho kuangalia namna ya kusaidia vyama vya msingi na vyama vikuu, ili viondokane na tatizo la unyevu na kuwapatia vifaa vya kuanikia korosho ili kukidhi viwango vinavyostahili,"alisema.

Kadhalika, alisema wiki ijayo Wizara hiyo inatarajia kugawa vifaa ambavyo vitasaidia zao hilo kuwa na ubora.

Awali, alisisitiza serikali itaendelea kutumia mfumo huo ili kuhakikisha minada inafanyika kwa wakati mmoja kwenye maeneo yenye msimu wa mavuno unaofanana ikiwamo Mkoa wa Pwani ili kuongeza ushindani wa bei na uwazi.

Sambamba na hilo, alisema kuwapo na mfumo wa uwekaji zabuni kwa njia ya sanduku kwa zao la Korosho.

# Fedha kupelekwa kwa awamu mradi wa maji Nanyamba

BUNGE limeelezwa kuwa tayari Wizara ya Maji itaendelea kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa Makonde uliopo mkoani Mtwara, ili utoe huduma kwa wananchi wa Nanyamba.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Nanyamba(CCM), Abdallah Chikota.

Katika maswali yake, Mbunge huyo alihoji serikali haioni ni wakati sasa wa kufanya mapitio ya usanifu wa mradi wa maji kutoka mto wa Ruvuma, kutokana na usanifu wake kufanyika zamani ili Maji yatoke Maembe chini na kupeleka Nanyamba na itasaidia kupeleka wilaya za jirani kama Tandahimba na Mtama.

"Ili kuboresha upatikanaji wa maji Nanyamba mradi wa Makonde ambao unanufaisha halmashauri nne lazima upatiwe fedha za kutosha za ukarabati, je, serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa wa mradi wa Makonde ili Halmashauri za Nanyamba, Tandahimba na Newala mjini na vijijini wapate maji ya kutosha,"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Mahundi, alisema Wizara hiyo imejipanga kuhakikisha Nanyamba maji yanapatikana.

"Tunafahamu baadhi ya maeneo ikiwamo Nanyamba, tumeshatoa maelekezo kwa Wahandisi maeneo hayo na ukarabati huu unatarajiwa kuanza mapema iwezekanavyo, na mradi wa Makonde tutaendelea kupeleka kadri tunavyopata,"alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo serikali itaanza kutumia maji ya Mto Ruvuma kwa ajili ya kujenga miradi mikubwa ya maji ambayo itatatua changamoto za maji kwa Jimbo la Nanyamba na maeneo jirani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema mradi wa maji kutoka mto Ruvuma ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati ambapo serikali inatarajia kuanza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2021/22 kulingana na upatikanaji wa fedha.

Aidha, alisema kupitia Wakala wa Maji Vijijini na Mijini(RUWASA) ukarabati na upanuzi wa mradi wa maji kwenye vijiji vya Malongo na Migombani umekamilika na unatoa huduma kwa wananchi.

Vilevile, alisema visima viwili vimechimbwa, mtambo nyumba ya mitambo ya kusukuma maji, ulazaji wa bomba kuu kilomita 3.5, ujenzi wa tanki moja la ujazo wa lita 100,000 na ujenzi wa matanki mengine manne unaendelea kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji Nanyamba Mjini.

"Pia, utekelezaji wa miradi katika vijiji vya Ngonja - Chawi, Mayembejuu, Nyundo A na B, Nitekela na Misufini upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji,"alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 13, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12



Rais hataki madarasa ya chini ya miti

ELIMU

# Mradi maji Victoria utakavyoongeza ari mpya kwa wasichana kitaaluma

**NA MARCO MADUHU, SHINYANGA**

WANAFUNZI wa kike wanaosoma shule za vijijini hasa za kata, wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi katika kutimiza ndoto zao za kufanikiwa kitaaluma, mojawapo ya matatizo hayo ni kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni, uhaba wa mabweni na ukosefu wa maji safi na salama kwa wanaoishi mabwenini.

Sera ya maji ya mwaka 2002, inaeleza kuwa ifikapo mwaka 2025 asilimia 85 ya wananchi wa vijijini watapatiwa maji safi na salama huku wakazi wa mijini watakuwa wamepata huduma hiyo kwa asilimia 100.

Kwa kuona umuhimu wa kufikia azma hiyo, serikali mwaka 2019 ilianzisha Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), kwa lengo la kuongeza ufanisi na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo hayo na kuyafikisha kwenye taasisi za serikali, zahanati, vituo vya afya, pamoja na shuleni na mabwenini pia ili kuondoa changamoto mbalimbali zitokanazo na ukosefu huduma hiyo.

Shule ya Sekondari Masengwa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ilianzisha utaratibu wa wanafunzi wa kike kuishi bwenini, ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu, pamoja na kuwaepusha na vishawishi na hadaa za wanaume wakitoka shule.

Licha ya wanafunzi hao kukaa bweni wameendelea kukumbana na changamoto za kulaghaiwa na wanaume, sababu ya kufuata huduma yakiwamo maji safi umbali mrefu katika kijiji jirani cha Mwamatongo na kujikuta baadhi yao wakiingia kwenye mitego ya mahusiano ya kingono na kisha kupewa ujauzito na kuacha shule.

Mwanafunzi Eta Elison, anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Masengwa anayeishi bweni anasimulia adha ambayo wanaipata kutokana ukosefu wa maji safi na salama karibu na shule.



Wananchi wakifurahi maji yalipofika kijijini kwao. **PICHA: MARCO MADUHU**..

> Pia tunapofuata maji haya umbali mrefu tunachoka sana hata kushindwa kujisomea vizuri sababu ya kutembea yote hayo husababisha kushuka kitaalamu ...

Anasema wanapokuwa wakifuata huduma hiyo kijiji jirani cha Mwamatongo, hukumbana na wanaume ambao baadhi yao hujikuta wakiingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na kisha kuambulia ujauzito na kukatisha masomo kutokana na hadaa za wanaume.

"Pia tunapofuata maji haya umbali mrefu tunachoka sana hata kushindwa kujisomea vizuri sababu ya kutembea yote hayo husababisha kushuka kitaalamu tofauti na matarajio yetu ya kuendelea kuongoza kwenye mitihani na kuwashinda wavulana,"anaongeza Eta.

Aidha, anasema kuanza kwa mradi wa maji safi na salama shuleni hapo, ambao unatekelezwa na RUWASA, itakuwa mkombozi kwao kutimiza ndoto zao, sababu ya kuondokana na adha ya kusaka maji umbali mrefu.

Takwimu za mwaka 2012 zinaitaja Shinyanga kuwa inaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora asilimia 58, ya tatu ni Mara asilimia 55 yote hayo husababisha watoto kuzima ndoto zao pale wanapopewa ujauzito na kuacha masomo.

Mkuu wa Sekondari ya Masengwa, Salu Jackson, anashukuru kufikiwa na mradi huo wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria shuleni hapo, ambao utaondoa changamoto za mimba kwa wanafunzi, pamoja na kupandisha shule kitaaluma zaidi.

Anasema kutokana na ukosefu wa maji safi na salama shuleni hapo, wanafunzi wa kike ambao wanaishi bweni hukumbana na changamoto nyingi wakati wakiwa njiani kufuata maji hayo.

"Takwimu za mwaka 2020, wanafunzi wawili walipewa ujauzito, ambapo na mwaka huu wengine wawili wameshapewa ujauzito na kuacha masomo," anasema Jackson.

"Licha ya kukumbana na changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama shuleni hapa, wanafunzi hawa wa kike wamekuwa wakifanya vizuri pia kitaaluma kuliko wavulana sababu ya kuishi bweni," anaongeza Mwalimu Mkuu.

Aidha, anataja matokeo ya kidato cha nne mwaka jana ya kidato cha nne shuleni hapo, kuwa ufaulu daraja wa kwanza walipata wasichana watatu tu, daraja la pili walipata wasichana 11 na wavulana tisa, daraja wa tatu walipata wasichana tisa na wavulana tisa, na daraja la nne wasichana walikuwa 32 na wavulana 11.

Aziza Joseph ni mama ambaye anaishi Kijiji cha Masengwa anasema mradi wa maji kwenye kijiji hicho, licha ya kuwa mkombozi kwa mabinti zao kuwaepusha kufuata maji umbali mrefu na kukutana na vishawishi vya wanaume wanaowapa ujauzito, utawapunguzia tatizo la kupoteza muda na kuwawezesha kufanya shughuli za kiuchumi.

Anasema mradi huo wa maji utakapokamilika ukichukua maji kutoka Ziwa Victoria, utakuwa mkombozi kwenye kijiji hicho na utawaepusha pia wanawake kuamka saa 11 alfajiri kufuata maji, kukumbana na wanyama hasa fisi na kuhatarisha maisha yao.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) mkoani Shinyanga, Juliet Payovela, anasema mradi wa maji katika Kijiji cha Masengwa ulianza kujengwa Novemba mwaka jana na unatarajiwa kukamilika na kuanza kutoa huduma ya maji kuanzia mwezi Machi.

Anasema mradi huo wa maji unaogharimu Shilingi milioni 234, umeshasambaza gata na mikingio ya kuchotea maji kijijini humo na katika Sekondari ya Masengwa ili kuwaondolea adha wanafunzi hao kufuata maji umbali mrefu na kupoteza wakati huku baadhi wakitumbukia kwenye vishawishi vinavyowaingiza kwenye majanga ya mimba za utotoni.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Rais hataki madarasa ya chini ya miti

- Halmashauri, kamati, bodi zianze kazi



Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Samiah Suluhu Hassan . **PICHA: MAKTABA**



Wanafunzi wanaosoma chini ya miti wapo kwenye hatari za kuumwa na nyoka, kulowa wakati wa mvua na hata kuumizwa na radi , ndiyo maana Rais anataka hali hiyo iishe sasa. **PICHA: MTANDAO**

LICHA ya juhudi zinazofanywa na serikali kumaliza kero mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu, hasa shule za msingi na sekondari, bado ukosefu wa miundombinu ya kusomea na kufundishia unaendelea kukwamisha jitihada hizi kwenye maeneo mengi nchini.

Uhaba wa madarasa unaosababisha wanafunzi kutoanza masomo kwa wakati, kusomea chini ya miti, wengine kwenda shule kwa zamu na pia kulundikana darasani ni kero zinazoripotiwa.

Uhaba huo wa madarasa ulisababisha wanafunzi 74,166 sawa na asilimia 8.9 wakiwamo wavulana 34,861 na wasichana 39,305 kutopangiwa shule katika awamu ya kwanza, kwa mujibu wa Ofisi ya Rais Tawala wa Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Aidha, wanafunzi 759,706, walifaulu wakiwamo wavulana 368,174 na wasichana 391,532 walichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021, lakini baadhi yao wakakwama kuanza masomo kwa wakati, TAMISEMI inaongeza.

Sasa Rais Samia Suluhu Hassan, anatoa maagizo kwa serikali na wizara nyingine kuhakikisha hakuna mtoto wa Tanzania anayesomea chini ya mti kwa sababu ya uhaba wa madarasa.

Waziri Ummy Mwalimu, mwenye dhamana na TAMISEMI, anasema hayo wiki iliyopita, mbele ya watendaji wa wizara hiyo jijini Dodoma: "Rais amenielekeza hataki kuona mtoto yeyote akisoma chini ya mti, kwa hiyo sisi TAMISEMI ni lazima tutekeleze, ameniambia mimi ni mama sitaki kuona mtoto wa Mtanzania akiwa chini ya mti."

> "Ninapata tabu sana kuona watoto wanakaa 200 katika darasa moja na baadhi ya shule watoto wanabadilishana wengine wanakuja asubuhi na wengine mchana kutokana na uhaba wa madarasa. Siamini katika hilo...

Anasema, pamoja na maagizo ya Rais, yeye pia hafurahii kuona wanafunzi wanasoma kwa zamu au chini ya miti kutokana na uhaba wa madarasa na anatamani shule ziwe na madarasa ya kutosha kwa wakati.

**HILI PIA TATIZO**

Mbali na wanafunzi kusomea chini ya miti au kwa zamu, Waziri Ummy anataja kero nyngine ambayo inachangia kupunguza uelewa wa wanafunzi kuwa ni mlundikano wao madarasani.

"Ni lazima tubadilishe hali hii kwa kujenga madarasa ya kutosha, inasikitika kuona baadhi ya shule zina mlundikano mkubwa wa wanafunzi madarasani, hali ni hatarishi kwa wanafunzi na inapunguza uelewa wao," anasema Ummy.

Ummy anawataka watendaji wakuu wa wizara hiyo kuanza utekelezaji wa maagizo ya rais ili kuondoa kero mbalimbali katika shule ikiwamo mlundikano wa wanafunzi madarasani, kuboresha mazingira ya kujifunzia.

"Ninapata tabu sana kuona watoto wanakaa 200 katika darasa moja na baadhi ya shule watoto wanabadilishana wengine wanakuja asubuhi na wengine mchana kutokana na uhaba wa madarasa. Siamini katika hilo, kwa kuwa watoto wanaoingia mchana hawawezi kuwa makini katika kusoma. Lazima tubadilishe kwa kujenga madarasa vya kutosha," anasema.

Waziri huyo anasema, mbali na hayo, kuna haja pia kwa kila shule kuwa na maabara na nyumba za walimu, kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia.

"Ni wakati sasa wa kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kutatua kero hizo, kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri ili zifanye kazi hizi muhimu katika kukuza sekta ya elimu nchini," anasema.

**MAZINGIRA BORA**

Kwa kawaida mazingira ya kujifunzia, ndiyo ambayo yanaweza kuwashawishi wanafunzi waipende shule yao au waichukie, hivyo kuboresha mazingira ni jambo la muhimu katika elimu.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, elimu bora hupatikana katika mazingira bora, yakiwamo ya kujifunzia na kufundishia, ambayo yanawafanya wanafunzi wawe na utulivu wanapofundishwa.

Rais ameshaagiza kuwa hataki kuona mtoto wa Kitanzania anasomea chini ya miti, kwa kuwa anajua kero zinazotokana na mazingira hayo ambayo si rafiki kwa maendeleo ya kielimu ya mwanafunzi.

Watendaji na wadau wote wa elimu, ni vyema wakahusika katika kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia ili kusaidia watoto kupata elimu bora itakayowasadia katika maisha yao ya baadaye.

**AGIZO LA WALIMU**

Kabla ya kusema hataki kuona watoto wanasomea chini ya miti, Rais Samia alianza kwa agizo la kuitaka TAMISEMI kuajiri walimu 6,000 ili kuziba nafasi za wale waliostaafu au kufariki dunia.

Anatoa agizo hivi karibuni katika hotuba yake mara baada ya kuwaapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi mbalimbali, Ikulu jijini Dar es Salaam.

"Kuna mahitaji ya walimu zaidi ya 6,000, Utumishi mpo hapa naomba muajiri hao walimu wakatoe huduma kwa Watanzania, hivyo basi TAMISEMI na Utumishi mkashughulike na hilo mara moja", Rais Samia anasema.

Rais anasema, TAMISEMI ina jukumu kubwa la elimu na afya za Watanzania, na kuitaka ikamilishe miradi ya elimu, hasa shule za sekondari za wasichana.

**UHITAJI ULIPOANZIA**

Kutokana na uhaba huo wa walimu, katika mwaka fedha wa 2019/2020, serikali ilikuwa na mikakati mbalimbali ya kumaliza tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kuomba kibali cha kuajiri walimu 6,000.

Mkakati mwingine ulikuwa ni kuchukua walimu zaidi 11,000 kutoka sekondari na kuwashusha wafundishe katika shule za msingi ili waweze kuziba nafasi ya uhaba wa walimu katika shule hizo za umma.

Hiyo ni kwa mujibu wa aliyekuwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mwita Waitara wakati akijibu swali bungeni.

Hata hivyo, inaonekana kuwa tangu wakati huo, walimu 6,000 walikuwa bado hawajaajiriwa, ambapo Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza hilo lifanyike haraka kwa ajili ya kuendelea kuboresha elimu nchini.

ELIMU/KIUCHUMI

NA ANI JOZENI

# Serikali inapobaini hakuna mbadala wa wawekezaji



Uwekezaji wa kuzalisha nishati ni moja ya maeneo yanayohitaji mitaji na teknolojia kutoka ughaibuni. **PICHA: MTANDAO**

MWASISI wa fikra za mapinduzi na ujamaa, Karl Marx, aliwahi kusema zama mpya zinapoingia zinavaa mavazi ya zamani, hivyo kile ambacho ni kipya hakionekani ila cha zamani, kwani watu hawatungi lugha wanapoingia katika enzi mpya. Wanatukuza yaliyotangulia ambayo yalikwama mahali fulani.

Lengo ni ili wafikie kilele cha matazamio hayo, yaliyochimbiwa katika utamaduni wa siasa wa nchi husika, na kimsingi ukiangalia inakuwa hivyo kila mara. Maandiko ya Mfalme Suleimani yanasema hakuna jipya chini ya jua kwani dhamira na hisia zote zinachotwa katika kile kilichotangulia, kilichotukuka.

Ukiangalia mabadiliko yaliyoanza nchini hivi sasa unapata picha ya taifa kutoka katika awamu ya kwanza kuingia awamu ya pili, ambayo ilifanya kazi kubwa ya kuibadili Tanzania kutoka katika mkwamo wa ujima au ujamaa kuingia utandawazi, kila aina ya bidhaa kupatikana na vijana, kinamama kujajiri kwa urahisi kwa mpangilio huo. Mabadiliko hayo yakakinzana na hisia za uzalendo zikikosoa chini kwa chini kile kinaachotendeka katika awamu ya pili, wakichukua soko huria kwa kuangamiza mashirika ya umma ambayo yalijaa hasara na ubadhirifu uliokithiri. Ikaingia awamu ya tatu na ya nne, ikaboresha.

Ila awamu hizo ziligubikwa na mwelekeo wa vyama vingi usio na ushindani wa kiitikadi kuhusu sera na mwelekeo wa uchumi, kwani chimbuko la makundi yote hayo lilikuwa moja nalo ni wanafunzi na waalimu wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hawa walelewa katika nadharia za ujamaa, mapinduzi na mipango ya uchumi kama dini na uchumi wa soko kwao si fikra ya maisha ila mchepuo wa kiitikadi wa dhana za uchumi, unaopendelewa na wale waliotawala na kukandamiza nchi masikini.

Hisia hii ilijijenga kuanzia 1996 wakati mabadiliko ya awamu ya pili yanaanza, ikapata sauti baada ya miaka saba, 1993. UBINAFSISHAJI / WAWEKEZAJI

Licha ya kuwa awamu ya tatu ilijaribu hapa na pale kubinafsisha, hisia yake tangulizi ilikuwa ni kulinda mali za umma (mashirika makubwa hata kama hayapati faida) zisichukuliwe na wageni, hivyo kuweka mtego wa kubinafsisha. Dhamira ilikuwa ni kuituliza Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kuwa suala la ubinafsishaji bado lipo, ila katika hali halisi waliweka mazingira yasiyowezesha ubinafsishaji, kwa mfano kuuza asilimia 35 ya hisa, mgeni aingize fedha zake ila asiwe na uamuzi wowote, ilivyokuwa kwa Kampuni ya Simu (TTCL).

Kwingineko mgeni aliuziwa asilimia 49 lakini mwenyeji haingizi mtaji, ila anataka asilimia 49 ya faida mfano ilitoke kwenye Shirika la Ndege ATC iliyobinafsishwa na kuitwa ATCL, wakashindwana na hata ilipopanda kuwa asilimia 51 mathalani Shirika la Reli wakati huo TRL, hali ilibaki ile ile. Ubinafsishaji wa asilimia 70 wa Kampuni ya Bia (TBL) au asilimia 60 kwa kampuni ya Sigara (TTC) ni baadhi ya kazi zilizofanywa na awamu ya pili.

> Kwa Tanzania, Rais Nyerere hakuwa muumini wa nadharia ya Babu lakini alimruhusu apite aifundishe kwani Nyerere alikuwa na heshima kubwa kwa Jamhuri ya Watu wa China na asingedharau wameingia katika hatua gani ya sera za uchumi.

Wakati 'michezo' hiyo ya ubinafsishaii inaendelea, tayari ilikuwa imepita nadharia hapa nchini, kama wimbi tu la kiitikadi, lililoletwa na Profesa Abdulrahman Mohamed Babu, mwamanapinduzi wa Zanzibar aliyekuwa Waziri wa Biashara na Viwanda (Muungano) hadi Rais Abeid Karume alipouawa mwaka 1972.

Ila kutokana na chama cha Umma kilichoungana na Afro-Shirazi wakati wa mapinduzi kuongozwa na Babu ambaye kwa hulka za Zanzibar alikuwa Mwarabu, alitupiwa zigo hilo.

Nadharia hiyo haikuwa ya Babu kivyake tu ila alielewa alichokuwa anafanya kiongozi mkuu wa China wa awamu ya pili, Deng Xiaoping, kutumia ubepari kujenga ujamaa, yaani kuweka eneo la pwani (mashariki) ya nchi hiyo chini ya mfumo tofauti, ambako wageni wanaingia ubia na wawekezaji wa China kujenga taasisi kubwa za uzalishaji mali.

Kwa njia hiyo China sasa inaitetemesha Marekani kwa nguvu za uchumi na imekamata soko la dunia katika maeneo maridhawa na pia ni mjenzi mkubwa zaidi wa miundombinu kote duniani, hasa kutokana na kukua kwa uwezo wake kiteknolojia na mitaji mikopo ya riba ndogo sana ya mabenki ya kitaifa na nguvu kazi makini kwa unafuu. Inashinda zabuni kote duniani. Marekani inatweta kwa jambo hilo lakini haina jibu, kampuni yake ni ghali mno kwa mifuko ya wanaotoa zabuni.

Kwa Tanzania, Rais Nyerere hakuwa muumini wa nadharia ya Babu lakini alimruhusu apite aifundishe kwani Nyerere alikuwa na heshima kubwa kwa Jamhuri ya Watu wa China na asingedharau wameingia katika hatua gani ya sera za uchumi. Hiyo ilikuwa mwaka 1981 na 1982, Babu akafaulu kupata wafuasi kadhaa licha ya kuwa hawakujitangaza waziwazi lakini fikra yake ikaenea kwa baadhi ya makada wa CCM.

Alipoingia tena madarakani mwaka 1983 baada ya kugundulika mpango wa kupindua serikali, kufuatia ulalamishi wa mkwamo wa ujamaa, Edward Sokoine alikuwa na cheche za aina hiyo, ila chache, alisema suala siyo kuwa tajiri ila unapataje huo utajiri, akimaanisha usiwe ni wizi serikalini.

Aliyekuwa mfuasi wa Babu kwa dhati licha ya kuwa hakusema hivyo ni Ali Hassan Mwinyi, ambaye alifuta 'miiko ya uongozi' katika CCM ili watu wafanye biashara kujikimu, hata kujiendeleza kimaisha, isiwe taabu. Jambo hilo liliwaumiza wakereketwa wa CCM ambao kwao miiko ya uongozi ilikuwa lazima, ili watu wote wawe sawa, siyo wajineemeshe uraiani halafu serikalini na katika chama wazuiliwe kupata fedha.

Ndicho kilichotokea awamu ya tatu na ya nne, milango ikafunguliwa watu kujineemesha kote, na kwa vile fursa zao zilikuwa hazilingani, hata pale serikali ilipounda miradi ya maana kwa njia za mkato wakadai watu wanajitajirisha, serikali ikaona haya kujieleza, upinzani ukajitanua hadi kilele, 2015.

**MAGEUZI YA SASA**

Mwalimu Nyerere kwa upande huo alikuwa muumini wa mfumo wa vyama vingi, ila si wa mageuzi halisi ya uchumi, fikra yake hapo ikiishia katika kuuza mashirika yanayopata hasara, siyo yenye faida kama TBL, TCC wakati huo, suala ni kufungua milango, kuzuia ukiritimba, kupanua uchumi.

Awamu ya tano ikawa ndiyo kilele cha mgongano wa mikondo yote hiyo, kwanza ikiiona kuwa watangulizi wake walilea upinzani unaohatarisha umoja wa nchi kwani haujengi umoja huo kwa msingi wa sera tofauti ila unatafuta mizozo, ukitumwa au kuchochewa na makundi ndani ya CCM. Ndiyo hali aliyoikuta hayati Dk. John Magufuli akapambana nayo, akaweka malengo ya 'Tanzania Mpya.'

Kwa msingi huo mabadiliko ambayo mageuzi ya sasa yanalenga ni kushirikiana na wawekezaji kwa njia ya uwazi na udhati wa kutaka vitega uchumi, kwani wakereketwa wa mapinduzi walipuuza fikra ya Babu na hasa Deng, na kuponda sera za Rais Mwinyi, hawana majibu ya ukosefu wa ajira ila kusema 'fanya kazi.'

Katika kilimo, utandawazi, ambako bei ya mazao iko chini sana na walio wengi wanatazamia kujikimu kwa ajira za hapa na pale, hakuna mbadala kwa uwezekaji na siyo mtindo wa 'najificha nitafute' kama awamu ya tatu na ya nne ambao pia unachochea rushwa. Ni kuweka mazingira ambako serikalini kuna nidhamu ya matumizi ya fedha, siyo ubadhirifu na matanuzi, halafu biashara nayo inashamiri, si kubana sekta binafsi kwa vile serikalini wamebanwa, hivyo warudi serikalini kuomba vibali ili baadhi watumishi watumie ujanja kujinufaisha.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Mapenzi na huruma ya Blandina kwa watu wanaoishi na ulemavu



Blandina alikuwa mwana harakati wa ukombozi wa wanawake na watoto na mtetezi kinara wa wanaoishi na ulemavu.

MWISHONI mwa mwezi Machi mwaka huu, ulihitimishwa maisha ya mwanahabari Blandina Sembu, mtangazaji wa kipindi cha Jarida la Wanawake cha ITV.

Kifo chake kimetokana na mauaji na polisi wanaendelea na uchunguzi, mwili wa mwandishi wa habari wa ITV na Radio One Blandina, uliokotwa katika eneo la njia panda ya ITV na Bagamoyo Road Mikocheni jijini Dar es Salaam.

Kukiwa na maelezo kuwa ulitupwa na watu wasiojulikana waliodaiwa kuwa walikuwa wamempakiza kwenye gari la Noah na kuutupa sehemu hiyo.

Blandina alikuwa mwana harakati wa ukombozi wa wanawake na watoto na mtetezi kinara wa wanaoishi na ulemavu.

Siku za uhai wake alifanya mahojiano na Nipashe na katika mazungumzo hayo, sehemu kubwa ilihusu kuwatia moyo na kuwasaidia watu wanaoishi na ulemavu.

Itakumbukwa Blandina aliishi na ulemavu uliosababishwa na ajali iliyoondoa mkono wake.

Alisema kuna mengi yanayowapa changamoto wenye ulemavu na kubwa ni hali ya unyanyapaa kutoka kwa jamii inayowazunguka, ambayo alisema kuondoa hali hiyo ndiko kutakakofungua milango ya wanaoishi na ulemavu.

Anatoa mifano akisema watu wengi wanapoanza kuifahamu dunia na mazuri yake wanakuwa na hisia, fikra na ndoto za kuwa na mwenza.

Anasema awe mwanamke au mwanamume kila mmoja anaota kufunga pingu za maisha na mtu anayempenda, kuwa na watoto na kuishi maisha ya familia yenye furaha.

Ni matarajio na matamanio ya wengi, licha ya kwamba mambo ya ndoa na kukutana na mwenza sahihi hayatabiriki na zama hizi yanaelekea kuwa masuala yasiyo na uhakika.

"Lakini, kwa mwenye kuishi na ulemavu maisha yanakuwa na changamoto zaidi na suala la kufikia maisha wanayoyatamani huwa ni gumu zaidi kwa vile kila anayekutazama anakuona kama kuna mambo hayajatimia," anasema Blandina Sembu.

Ni katika mahojiano yake na Nipashe alipozungumza na safu ya Anayemulikwa, anasema watu wanaoishi na ulemavu wanastahili upendo, faraja na kupewa moyo zaidi bila kuchukuliwa kama watu wenye upungufu.

Iwe shuleni, vyuoni na ndani ya jamii wanahitaji kukubaliwa na kuonekana watu kama wengine kwa vile wako sawa na binadamu wengine.

Anasema, kama walivyo kinamama wengine wenye viungo vilivyokamilika, anayeishi na ulemavu anatamani kuwa na familia, wenza na watoto.

"Lakini utashangaa unayeishi na ulemavu, ukiwa mjamzito ukifika kliniki sura za wahudumu wa afya zinabadilika.Ukiingia kwenye wodi ya uzazi wanakushangaa zaidi. Unaweza kusoma sura zao wakijiuliza imekuwaje? Hata wewe umefikia hatua hii ...?" anasema kwenye makala iliyoandikwa na Anayemulikwa.

Anasema wakati mwingine mwenye ulemavu anaweza kukereka na kuchukizwa na hali hiyo na akaamua hata kutokwenda hospitalini hasa kina mama ambao wanaona au kuhusika hawakubaliki.

Alishauri kuwa na sehemu maalumu za kupokea na kuwahudumia kinamama wajawazito wanaoishi na ulemavu.

Alishauri wodi za uzazi ziwe na uwezo na wataalamu wa kuwasaidia wenye ulemavu wa viungo, wasioona, wasiosikia na wenye ulemavu mchanganyiko. Wawapo matabibu na wataalamu wanaofahamu lugha za alama na saikolojia,wenye upendo na wanaowapokea wenye uhitaji maalumu katika mikono salama na huruma kwa vile ni haki yao.

Blandina alikumbusha kuwa kukosa baadhi ya viungo kama mikono, miguu na macho kunawafanya wengine kuwakwepa wanawake wenye ulemavu.

"Naomba tujue kuwa ni vyema kufahamu kuwa haiwezekani kubadilisha maumbile kama umezaliwa bila uoni huwezi kuutengeneza, ukiwa na ulemavu mchanganyiko huoni, umelemaa viungo na pia husikii huwezi kubadilisha hali hiyo. Utatumia vifaa saidizi lakini huwezi kujibadilisha.

"Watu wenye ulemavu wanahitaji kupendwa na pia kupenda, kuwa na maisha bora kuheshimiwa ili wajikubali na kujiona kama wengine kwenye jamii," alisema Blandina.

Anakumbusha kuwa wapo watu wanaopenda kuwahadaa wenye ulemavu kwenye uhusiano na kwamba ni vyema wanaofanya hivyo wakafahamu kuwa hakuna anayestahili kuwa na uhusiano usio na uaminifu awe mwenye viungo vilivyotimia au asiye navyo na kwamba wote wanafurahia na wangependa kuwa na uhusiano wa kudumu na endelevu.

Anasema haipendezi kuwafanya wenye ulemavu kuwa kama 'doli' au matoi na kusisitiza kuwa wenye ulemavu hawataki wajisikie kuwa wako tofauti au wenye upungufu.

Blandina akitoa ushauri kwa wanaoishi na ulemavu anasema ni vizuri kuishi kwa kujiamini na kujitegemea na pia kuwa na hisia chanya wakati wote .

"Fanya kila unachoweza . Kifanye vizuri na kwa ukamilifu . Kuwa na matumaini, lakini usisubiri au kungoja eti jambo fulani litatokea jitahidi chukua hatua. Kama ni elimu ingia katika masoko yako. Jiwekee mipango mizuri kuwa na fikra chanya, uthubutu na uendelee kujiamini,"alisema .

Alikumbusha kuwa mwenye ulemavu hana sababu ya kufikiria kuwa anawafurahisha wengine ni lazima aifurahie nafsi yake kwani hawezi kubadilisha hali yake. Aanze kujipa furaha, kujiambia kuwa ninaweza na kujikumbusha kuwa atafanikiwa na hana haja ya kuwasikiliza na kusononeka na maneno ya wengine kuhusu yeye.

"Ni vyema kuachana na dhana na hofu kuwa ulemavu mtu alionao unaweza kuwa kikwazo kwenye mafanikio yako. Usiache fursa zinazotokea kwa sababu hufahamu lipi litakuwa na mafanikio." Anasema Blandina.



# Walimu waandaliwa kibano cha utoro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amemuagiza Katibu Mkuu (Prof. Riziki Shemdoe), kuangalia namna ya kuweka mfumo wa kisasa wa mahudhurio ya walimu kwa alama kidole ili kudhibiti utoro.

Pia, ameagiza kuanzishwa kwa madawati ya ulinzi wa watoto shuleni na kulinda haki za watoto wakiwamo watoto wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU).

Waziri Ummy aliyasema hayo jijini hapa, wakati wa kufunga mkutano wa kwanza wa umoja wa maofisa elimu kata.

Aliwataka maofisa elimu kata kusimamia mahudhurio ya wanafunzi na mahudhurio na ufundishaji wa walimu na kutosita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu.

**Chukueni hatua kwa walimu wanaoshiriki vitendo vya ukatili ikiwamo ukatili wa kingono kwa watoto, watu hawa tusiwaonee aibu.**

"Muhimu katika mahudhurio ya walimu, Katibu mkuu tuangalie kama walimu wetu wanaingia saa ngapi na wanatoka saa ngapi na utumiaji wa muda kikamilifu walimu wanapoingia kufundisha kama tunaweza kuanza na shule chache tufunge biometrick (mfumo wa kisasa wa alama za vidole) ili kudhibiti maudhurio ya walimu mashuleni," alisema.

Aidha, alisema pamoja na kuwapo na ongezeko la ufaulu kuanzia ngazi ya shule ya msingi hadi sekondari, bado kuna wanafunzi wasiomudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na wale wanaoshindwa upimaji wa taifa wa darasa la nne na kidato cha pili na kuwataka maofisa elimu kufanya usimamizi mzuri wa walimu ili kuondoa tatizo hilo.

Kuhusu vitendo vya ukatili kwa wanafunzi, Waziri huyo alisisitiza kutoonea aibu mwalimu anayeshiriki au kuwa wakala wa vitendo vya ukatili kwa watoto mashuleni.

"Chukueni hatua kwa walimu wanaoshiriki vitendo vya ukatili ikiwamo ukatili wa kingono kwa watoto, watu hawa tusiwaonee aibu, watoto tuwaache wasome, na huu ni ujumbe wangu kwa walimu wote na walimu ambao ni wakala wa watu wanaoshiriki vitendo vya ukatili kwa watoto," alisema.

Akizungumzia uhaba wa walimu kwa shule za vijijini, Waziri Ummy, aliwataka maofisa hao kuhakikisha hawaidhinishi uhamisho kwa walimu wasiokuwa na sababu za msingi.

Naye, Katibu Mkuu, Prof. Shemdoe aliwataka maoafisa elimu kata kujituma na kutekeleza wajibu wao ipasavyo ili kusaidia kuboresha elimu.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweri, alisema kuanzishwa kwa umoja huo ni jukwaa muhimu la maofisa hao kuwasilisha ushauri na kero zao na kupendekeza namna ya kuzitatua.




Maofisa elimu maalumu na walimu wa michezo kwa watoto wenye ulemavu wa akili, wakimsikiliza Mkurugenzi wa Special Olympics Tanzania, Charles Rays, ambae pia ni mkufunzi wa mafunzo maalumu ya michezo jumuishi iliyoandaliwa na Special Olympics Tanzania chini ya ufadhiri Stavros Niarchos Foundation (SNF) iliyofanyika Dodoma leo (jana). **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Masaju ashauri wazazi maendeleo taaluma ya watoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa serikali mstaafu, Jaji George Masaju, amewataka wazazi na walezi kutenga muda wao kufuatilia maendeleo ya masomo ya watoto wao, badala ya kutumia wakati mwingi mitandaoni.

Jaji Masaju ametoa rai hiyo alipokuwa akizungumza na wazazi, walezi na wanafunzi kwenye mahafali ya tatu ya kidato cha sita mwishoni mwa wiki katika Shule ya Sekondari ya Dodoma Central jijini hapa.

Alisema hivi sasa wazazi wengi wamekuwa wakitumia muda wao mrefu kuangalia mitandao na vipindi vya televisheni, badala ya kukaa na watoto wao kujua maendeleo ya masomo. Alibainisha kuwa wazazi hao wamekuwa wakidhani kuwa wakulaumiwa ni walimu.

"Yaani wewe mtoto unamhangaikia,unamlinda na kumtafutia shule, lakini unashindwa kumfuatilia ili kujua mwenendo wake, akifanya vibaya lawama zote zinatupiwa kwa walimu wakati makosa yapo kwenu nyinyi wazazi na walezi," alisema Jaji Masaju.

Aliwataka wahitimu kuacha kuwa na ndoto za kutaka kuoa na kuolewa, badala yake waongeze bidii zaidi ya kutafuta elimu itakayowafanya wajiajiri wenyewe.

Mkuu wa shule hiyo, Hashim Swaib, alisema kwa sasa ipo katika nafasi nzuri kimasomo kutokana na ufaulu mzuri uliopo, ambapo kwa matokeo ya kidato cha sita mwaka jana waliweza kupata daraja la kwanza, la pili na la tatu na hapakuwapo daraja la nne wala sifuri.

Alisema kwa matokeo ya mwaka huu ana imani kubwa wanafunzi wake watapata ufaulu mzuri zaidi.

"Hapa naomba nisisitize na kuwahakikishia wazazi na walezi tutafanya vizuri kwa hao wanafunzi wa kidato cha sita, na mtoto yoyote ambaye atapata daraja la nne na sifuri, mzazi na mlezi ufike ofisini kwangu ili niweze kumrudishia karo yote ya mwanao nasema hivi kutokana na wanafunzi wangu nilivyowaandaa kimasomo," alisisitiza.

# Waziri ataja mkakati kuimarisha viwanda nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ameagiza mambo kadhaa kwa ajili ya kuimarisha sekta ya viwanda na biashara ili zichangie kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na menejimenti ya wizara na wakuu wa taasisi zilizopo chini ya wizara hiyo, jijini hapa.

Alisema Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 inalenga kuona Tanzania inahitimu na kuondokana na umasikini kwa kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, na kusisitiza kuwa ili kufikia dira hiyo ,wizara hiyo ina nafasi na mchango mkubwa.

Waziri huyo alisema katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Tatu, malengo sita kati ya malengo mahsusi 12 yanahusu sekta ya viwanda na biashara na kati ya vipaumbele vitano vya mpango huo vitatu vinahusu wizara hiyo.

Hata hivyo, Profesa Mkumbo alisema hakusudii kutumia muda mwingi katika kutunga sera, sheria na mikakati na kuwa yeye analenga katika utekelezaji na kuona matokeo ya utekelezaji huo kwa kuchochea ukuaji wa haraka wa sekta ya viwanda na biashara.

Aliwataka wataalamu wa idara ya sera na mipango na ile ya sheria kusimamia uhuishaji wa nyaraka mbalimbali za kisera ili ziende na wakati na kuakisi maudhui ya mpango wa maendeleo na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Prof. Mkumbo alitaka kuwekwa bayana dhana na aina ya viwanda vinavyotakiwa kuendelezwa nchini, kuwa na kanzidata ya kisasa ya viwanda na kupima maendeleo ya viwanda kwa kuzingatia uzalishaji na kiwango cha ajira.

Alisema pia kuimarisha utafiti na matumizi yake katika maendeleo ya viwanda, ikiwamo kuwa na ushirikiano wa karibu na taasisi za utafiti na elimu ya juu na kupanua na kuboresha uhusiano na ushirikiano na taasisi za sekta binafsi.

Waziri huyo alisisitiza suala la kujenga imani kwa wafanyabiashara kupitia, uwazi na kutabirika kwa mwelekeo wa kisera wa Serikali na mawasiliano chanya ya mara kwa mara.

"Natarajia kuwa kazi zote zitakazofanywa na Wizara ziwe na viwango vya hali ya juu kuanzia uamuzi na mikakati ili kuleta tija katika utendaji wa Wizara,"alisema.



# 'Marufuku wanufaika TASAF kukatwa ruzuku'

**Na Nebart Msokwa,** MOMBA

SERIKALI imepiga marufuku watendaji wake kuwakata fedha za ruzuku wanufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF) kwa lengo la kuwalazimisha kuchangia shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

Pia, watendaji hao wametakiwa kutoa elimu kwa wanufaika na kuwasaidia utaalamu wa kuendesha miradi wanayoanzisha ili istawi na kuwasaidia kubadili maisha yao kiuchumi kama ilivyo lengo la serikali.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratias Ndenjembi, alipofanya ziara ya kutembelea wanufaika wa mpango huo katika kata tatu za Wilaya ya Momba, mkoani Songwe.

Alitoa agizo hilo kwenye mkutano wa hadhara wa wanufaika wa Kata ya Chitete baada ya baadhi ya wananchi kulalamika kukatwa fedha zao kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo elimu na afya.

**Hatujapewa elimu ya kutosha kuhusu fedha ambazo huwa tunakatwa, kwahiyo tunaomba utusaidie maana huwa hatuelewi kabisa kwanini tunakatwa fedha hizo.**

Alisema fedha wanazopatiwa wanufaika hao ni za kwao na hawatakiwi kukatwa kiasi chochote na kwamba endapo kuna mchango wanatakiwa kuchangia unatakiwa kuwa wa hiyari na sio kulazimishwa kwa kuwa ni kuharibu malengo ya serikali.

"Hizo fedha tunataka ziwasaidie hawa wananchi, msiwalazimishe kuchangia michango, waacheni waanzishe miradi, wakiinuka kiuchumi watatuchangia michango inayotakiwa kwa hiyari yao, kama ni bima ya afya watachangia na kama ni shule watachangia, lakini msiwakataze," aliagiza Ndenjembi.

Aliwataka maofisa ugani wa vijiji kuwasaidia wanufaika kwenye uendeshaji wa miradi wanayoanzisha ili iwe endelevu na kuinua uchumi wa wanufaika hao.

Aliwataka wanufaika wa mpango huo kutumia fedha wanazopata kwa ajili ya kujiinua kiuchumi badala ya anasa ikiwamo ulevi na kuoa wanawake wengine baada ya kuzipata.

Awali, wanufaika wa Kata ya Chitete walimuomba Naibu Waziri awasaidie ufafanuzi wa fedha ambazo huwa wanakatwa kwa maelezo kuwa hawana elimu ya kutosha.

Mmoja wa wananchi hao, Bahati Simpasa, alisema wamekuwa wakikatwa fedha hizo na wakihoji wanaambiwa ni kwa ajili ya kulipia huduma za afya na elimu.

"Hatujapewa elimu ya kutosha kuhusu fedha ambazo huwa tunakatwa, kwahiyo tunaomba utusaidie maana huwa hatuelewi kabisa kwanini tunakatwa fedha hizo," alisema Simpasa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Momba, Condester Sichalwe, alisema kati ya vijiji 72 vya halmashauri hiyo, 26 ndivyo havijaingizwa kwenye mpango huo na kuiomba serikali iviingize kwenye bajeti ijayo.

Alisema kwenye vijiji ambavyo vinanufaika kuna baadhi ya wananchi wana sifa za kunufaika na mpango huo, lakini hawanufaiki kwa sababu mbalimbali na kuiomba serikali kuwaongeza.

"Katika Kata ya Msangano vijiji vyote havijaingia kwenye mpango huu, sasa kila nikikutana na wananchi hawa wanalalamika wakitaka na wao waingizwe ili waboreshe maisha yao, nakuomba Naibu Waziri utusaidie nao waingizwe," alisema Sichalwe.

Akijibu ombi hilo, Naibu Waziri Ndenjembi alisema vijiji vyote 26 vya jimbo hilo ambavyo havikuingizwa kwenye awamu zilizopita vitaingizwa kuanzia mwaka wa fedha ujao unaotarajiwa kuanza Julai mosi mwaka huu.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Uhawilishaji fedha kutoka TASAF Makao Makuu, Seleman Masala, alisema kabla wananchi hawajaanza kunufaika huwa unapitishwa kwanza mchakato wa kuchagua watu wanaostahili kunufaika ambao unaanzia kwenye ngazi vya vijiji.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratias Ndenjembi, akiwahutubia wananchi wa Kata ya Nkangamo katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba, mkoani Songwe, wakati alipofanya ziara ya kuwatembelea wanufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Masikini mwishoni mwa wiki (TASAF). **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Watumia nguvu zao kujenga barabara km 2

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Iwambi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wametumia nguvu zao kujenga barabara yenye urefu wa zaidi ya Kilomita mbili ili kurahisisha mawasiliano ya barabara kati ya eneo lao na maeneo mengine ya jiji.

Wananchi hao wameiomba serikali iwasaidie utaalam wa kuweka mitaro na makaravati ya kupitisha maji ili barabara hiyo idumu kwa muda mrefu na kuwa wameijenga barabara hiyo kwa kuchangishana fedha kwa ajili ya kukodi mitambo.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki wananchi hao walisema waliamua kujenga barabara hiyo baada ya kuona wanapata shida ya kusafiri kutoka katika eneo hilo kuunganisha katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).

Charles Mtagwaba, miongoni mwa wakazi wa eneo hilo alisema awali katika eneo hilo hapakuwa na barabara isipokuwa palikuwa na wigo uliokuwa unatenganisha shamba la mifugo na maeneo ya wananchi.

Alisema baada ya wananchi kuongezeka katika eneo hilo waliamua kuanza kulima barabara hiyo kwa kutumia jembe la mkono, lakini walikuwa wanashindwa kufanikiwa kwa sababu mafuriko yalikuwa yanazoa udongo na kusababisha makorongo.

John Chigazi, alisema wamejenga barabara hiyo kwa kiwango cha kawaida na wanaiomba serikali iwasaidie kuboresha zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka vifusi vyenye ubora na mitaro imara kwa kuwa hawana utaalamu.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kuunganisha makazi yao na barabara kuu ambayo inawaunganisha na eneo la katikati ya Jiji la Mbeya ambako ndiko huduma nyingi muhimu zinapatikana.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Jiji la Mbeya, Mhandisi Seleman Mziray, alisema barabara hiyo haimo kwenye mtandao wa barabara na wakala huo na kuwataka wananchi hao kuendelea kufuata taratibu.

Alisema wananchi hao wanatakiwa kuomba ili barabara hiyo ianze kuhudumiwa na TARURA huku akiwapongeza wananchi hao kwa kuamua kujenga barabara hiyo.

Alisema wananchi wanatakiwa kuanza na mikutano ya mitaa yao kisha wawasilishe mihutasari yao kwenye kata kabla ya kufikishwa kwenye vikao vya halmashauri.

## Wawekezaji wakumbushwa kuzingatia sheria za kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imewataka wawekezaji wa kigeni walioopo mkoani humo kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria za nchi ili kuepuka usumbufu unaoweza kukinzana na sheria za nchi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila mwishoni mwa wiki wakati wa kikao maalumu kati ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo, Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) na wawekezaji wenye asili ya China.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya wawekezaji ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa utulivu na kuchangia kupunguza tatizo la ajira na kuinua uchumi wa nchi.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan amesisitiza wawekezaji kupewa kipaumbele, sasa mimi nataka niwahakikishie kwamba katika mkoa wetu huu hakutakuwa na mkwamo wa aina yoyote ile, tumejipanga na wenzetu wa TIC pamoja na vyombo vya dola ili kusiwapo na matatizo," alisema Chalamila.

Alisema moja kati ya sheria ambazo wawekezaji wanatakiwa kuzingatia wakati wa uendeshaji wa kazi zao ni sheria ya kazi ambayo inasisitiza mikataba na mambo mengine ya kuzingatia wakati wa kutoa ajira.

Kwa upande wao baadhi ya wawekezaji hao waliishukuru serikali kwa kuwapatia ufafanuzi huo huku wakilazimika kuomba radhi kwa Serikali na Watanzania kutokana na tukio la hivi karibuni la mwenzao mmoja kumcharaza bakora mmoja wa Watanzania mkoani Mbeya.



# ‘Watendaji simamieni maeneo yaliyotengwa’

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa Baraza la Madiwani Mjini Magharibi wametakiwa kusimamia matumizi sahihi ya maeneo yaliyotengwa ya kijamii kutumika kama ilivyokusudiwa ili kuepuka kwenda kinyume na matumizi hayo.

Akifungua kikao cha Baraza hilo kwa robo tatu ya mwaka wa fedha 2020 – 2021 jana Katibu Tawala Mkoa wa Mjini Magharibi , Radhia Rashid Haroub, alisema kumekuwa na matumizi yasiyokuwa sahihi kwa maeneo yaliyotengwa kwa shughuli mbalimbali ikiwamo michezo kutumika kwa matumizi mengine ikiwamo kuegesha magari.

Alisema maeneo hayo yana umuhimu wake na serikali imeamua kuyatenga kwa shughuli hizo muhimu, hivyo kuendesha shughuli kinyume na ilivyokusudiwa ni kuharibu muonekano na haiba ya maeneo hayo.

Aidha, aliwataka kuendelea kusimamia usafi wa Jiji la Zanzibar kwani bado hali hairidhishi licha ya jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika.

“Jiji haliridhishi ingawa usafi unaendelea hivyo, wabuni njia zitakazoweza kufikia kiwango bora pamoja na kupanga mambo yenye faida kiuchumi pasipo kuingiliana na mamlaka nyengine,” alisema.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa robo mwaka Kaimu Mkurugenzi Baraza la Jiji, Said Salmini Ufuzo, alisema wameanza uandaaji wa miradi ya ubunifu ikiwamo matangazo kwa njia za kielektroniki na kufanya mazungumzo na Kamisheni ya Utalii na Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kuzibaini fursa za kiuchumi kupitia sekta ya utalii.

Wakichangia ripoti hiyo, madiwani wa baraza hilo, wameshauri kuangalia upya majukumu ya mamlaka za serikali za mitaa ili kuepuka migongano ya kazi zao na baraza la jiji na kusimamia vyema masuala ya ukusanyaji wa mapato.

# Hemed ataka usimamizi bora wa SACCOS

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa wito kwa Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuongeza kasi ya kuwaelimisha wananchi hasa katika kipengele cha usimamizi na uongozi wa vyama vya ushirika ili Taifa lisheheni SACCOS zilizo imara.

Hemed alitoa wito huo juzi wakati wa kuufungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Meli Nne Saccos katika Wilaya ya Magharibi ‘B’ ambao pamoja na mambo mengine, ulimchagua makamu mwenyekiti wake.

Alisema ushirika bado ni nyenzo muhimu ya kupambana na umaskini na ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka Ofisi ya Mrajis wa vyama vya ushirika katika kuhakikisha eneo hilo linaimarika na kusaidia uchumi wa taifa.

Alibainisha kwamba Zanzibar na Tanzania kwa ujumla zilikuwa na SACCOS nyingi zilizoanzishwa kwa lengo la kumkomboa mwananchi hasa yule wa kipato cha chini, lakini nyingi kati yao zilishindwa kuendelea kutokana na ubadhirifu pamoja na tatizo la uongozi.

**Tabia ya kuoneana haya katika eneo la fedha ndilo linalochangia kuanguka kwa mitaji na hatimae harufu ya kufilisika kwa Taasisi isiyo madhubuti inakaribia.**

Makamu wa Pili wa Rais alipongeza wanachama wa Meli Nne Saccos kwa maendeleo makubwa waliyoyapata tokea kuasisiwa kwa Saccos yao mwaka 2005 wakianzia na mtaji wa Sh.700,000 na hivi sasa wanajivunia kuwa na mtaji wa zaidi ya Sh. bilioni 3.7.

Alisema hayo ni maendeleo makubwa ambayo wanachama hao wana haki ya kutembea kifua mbele.

Hemed aliwaeleza kwamba uamuzi wa kuondoa tofauti zao na kujikusanya pamoja kwa kuunda chombo hicho wakizingatia umoja na mashikamano ndio uliowafikisha hatua ya mafanikio makubwa na kuwa mfano bora.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliwashauri wanachama hao kuelezana ukweli pale kunapotokea mapungufu yanayojitokeza wakati wa kupokea ripoti hasa katika masuala ya fedha eneo wanalopaswa kulichangia bila ya kigugumizi chochote.

Alisema kwamba tabia ya kuoneana haya katika eneo la fedha ndilo linalochangia kuanguka kwa mitaji na hatimae harufu ya kufilisika kwa Taasisi isiyo madhubuti inakaribia.

Akisoma risala mmoja wa viongozi wa Meli Nne Saccos, Amina Mohamed Waziri, alisema Saccos hiyo iliyodumu kwa takriban miaka 15 sasa ilianza na wanachama 150 wakati hivi sasa imeshafikisha 1,737 ikiwa na mtaji mkubwa wa zaidi ya Sh. bilioni 3.7.

Alibainisha kwamba jumla ya wanachama 3,726 wamepatiwa mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni 7.2 katika kuendesha shughuli za biashara, elimu masuala ya ujenzi, sekta ya kilimo pamoja na matibabu na tayari zaidi ya Sh. bilioni 5.4 sawa na asilimia 77zimesharejeshwa.

Akimkaribisha kuunfungua mkutano huo Mkuu wa Wilaya ya Magharibi ‘B’ kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hamida Khamis Mussa ,alisema inapendeza kuona uongozi wa Wilaya haujapokea tatizo lililoripotiwa kuvuruga mwenendo wa Saccos hiyo.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabaan, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani ) juu ya bei elekezi ya vyakula ikwamo mchele, unga wa ngano na sukari kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ofisini kwake Malindi Zanzibar. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# SMZ kufuatilia bei elekezi ya vyakula

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imesema itahakikisha inasimamia bei elekezi ya bidhaa za vyakula wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Juzi serikali ilitangaza bei elekezi kwa ajili ya bidhaa za vyakula vinavyotumika wakati wa mfungo wa huo unaotarajiwa kuanza leo kulingana na muandamo wa mwezi.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema lengo la kutoa taarifa hiyo ni kuwawezesha wananchi wenye kipato cha chini kumudu kununua bidhaa hizo.

Alisema kwa vile serikali inawapenda na kuwajali wananchi wake, itasimamia kuona bei iliyowekwa ndio itumike ili wamudu bidhaa muhimu zinazotumika katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Waziri huyo akitaja bei elekezi hizo alisema mchele wa mapembe utatakiwa usizidi Sh. 1,600 kwa kilo, sukari Sh. 2,000 kwa kilo na unga wa ngano usizidi Sh. 1,600 kwa kilo.

Pia alisema tabia za kutaka kuchuma faida kupita mgongo wa wanaofunga hazikubaliki na mara nyingi husababisha wananchi walio wengi ambao hali zao duni kutekeleza ibada ya funga katika mazingira magumu.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara na wananchi wote wazingatie bei elekezi ambayo Serikali imetangaza na wasipofuata hatua kali zitachukuliwa kwa wale watakaokiuka bei hizo.

HABARI KITAIFA

# CAG: Barabara mabasi mwendokasi ina nyufa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini dosari katika ujenzi wa miundombinu ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, maarufu mwendokasi, ikiwa ni pamoja na barabara zake kujaa nyufa.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa amebaini matatizo ya ubora kwenye tabaka la zege lililojengwa kwenye njia ya mabasi hayo.

Anabainisha kuwa kwa mujibu wa michoro na miongozo ya viwango vya ubora, tabaka la zege kwa ajili ya njia ya mabasi hayo ilitakiwa kuwa na unene wa milimita 220, upana wa mita 3.5 kwa tabaka la saruji la C1 na tabaka lililoboreshwa la udongo kiwango cha G15.

"Nilibaini barabara kuwa na nyufa kati ya kilomita 6.4 hadi 8.91. TANROADS (Wakala wa Barabara) iliamua kuchunguza sababu ya kushindwa kufikia ubora.

"Kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi, sababu kuu za kasoro hizo kwenye barabara ya zege zilihusishwa na usafirishaji duni wa zege kutoka kwenye sehemu inayohusika na uzalishaji hadi mahali pa kazi.

"Kutoka sehemu ya uzalishaji, zege lilisafirishwa kwa gari kubwa kisha katika sehemu ya kazi, zege lilibebwa kwa mtambo wa kuchimbia miundombinu na kuweka kwenye mtambo wa kusambaza zege. Hivyo, taratibu za ubebaji huu wa zege zilisababisha kutengana kwa zege.

"Sababu zingine zilizohusishwa na zege hilo kutoa nyufa zilijumuisha: mkandarasi kutotoa kwa kiwango cha kutosha udongo wa mfinyanzi na uchafu uliotokana na masalia ya mimea katika mchanga. Hii ilisababisha idadi kubwa ya mashimo kwa juu na ndani ya barabara ya zege.

"Sababu nyingine ni kwamba, mkandarasi kutobeba kwa kiwango cha kutosha vifaa vya ujenzi (mchanga, kokoto, saruji na zege) kutoka sehemu vifaa vilipokusanywa ili kuhifadhiwa (mchanga, kokoto) hadi sehemu ya kumwaga zege. Hii ilisababisha mchanganyiko usiofanana wa zege ambao baadaye ukatengeneza nyufa," anabainisha.

CAG anaendelea kubainisha kuwa uchunguzi ulibaini mkusanyiko wa vifaa vya ujenzi (mchanga, kokoto), utengenezaji wa kokoto za saizi kubwa na ubebaji wa mara kwa mara wa zege safi kabla ya kulimwaga ni sababu kuu zinazohitaji zitatuliwe.

"Nilibaini aina za nyufa zilizoenea upana wote wa barabara pasipo kuthibitika ni za aina moja. Vilevile, zilibainika nyufa zilizozama ndani kati ya maungio ya kuruhusu kutanuka. "Ukaguzi ulibaini hali hii ilitokana na kuchelewa kukatwa kwa maungio. Hata hivyo, nilibaini kwamba, TANROADS hawakuchukua hatua kali na stahiki kwa mkandarasi licha ya matatizo ya ubora yaliyojitokeza," anasema.

Katika ripoti yake hiyo, CAG anashauri menejimenti ya TANROADS kuhakikisha mkandarasi anarekebisha sehemu zote zilizobainika kuwa na ubora duni kabla hajaweka tabaka la kudumu la zege na kuchukua hatua kali kwa mkandarasi kwa kazi zote zilizofanyika chini ya kiwango.

CAG pia anasema amebaini huduma za uhandisi elekezi kwa ajili ya usanifu wa kilomita 42.9 wa Mabasi Yendayo Haraka - Awamu ya 2 na 3 ilicheleweshwa kwa miaka minne.

## Mbunge: Mgonjwa akikosa bima hospitalini aite polisi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba (CCM), amesema wananchi wenye bima za afya wakikosa dawa katika vituo vya afya, waripoti polisi kwa kuwa bima ni sawa na mchezo wa kamari.

Kishimba ambaye amekuwa akiibua hoja za kushtusha katika mijadala ya Bunge, alitoa kauli hiyo bungeni jijini Dodoma jana, alipochangia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/26).

Alisema haoni mahali mpango huo umetilia umuhimu afya kwa kueleza namna wananchi watakavyopata matibabu bure.

Mbunge huyo alisema matibabu na bei za dawa hazimgusi mwananchi maskini, akimwomba Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuongeza Sh. 30 au 40 kwenye mafuta ili kuwapatia matibabu bure Watanzania.

Alisema katika majimbo yao, hali ya umaskini ni mbaya, akifafanua: "Wananchi hawa kwa kuwa hawana tatizo la nyama, sukari, wanaipita nyama hapo wanakwenda kununua mchicha bila malalamiko. Wao tatizo lao ni dawa na kwa bahati nzuri ugonjwa hawawezi kujisakizia."

Alisema hadhani kuwa kuna serikali yoyote duniani iliwahi kutibu wananchi wake bure ikafilisika, akisisitiza kuwa nchi inaweza kufilisika kwa vita.

Kishimba alisema kwa mapato yaliyopo nchini, serikali ifikirie kuwatendea haki Watanzania.

"Tatizo la bima ni sawa sawa na kamari. Tunaona wacheza kamari mtu anapoliwa akiwa hana pesa, polisi wanakuja. Vipi anayekwenda hospitali na kuambiwa dawa hamna?

"Kwanini Waziri wa Mambo ya Ndani (George Simbachawene), asipunguze trafiki barabarani na kuhamisha baadhi ya polisi hospitalini ili mgonjwa mwenye bima anapoambiwa hakuna dawa aende akaripoti polisi ili anusuru uhai wake?" Alihoji.

Alisema kuwa nusu ya wabunge wanapokea simu kutoka kwa wapigakura wao wakipata malalamiko kuhusu dawa na matibabu.


# VARIOUS JOB VACANCIES

Mwiba Holdings Limited is a registered Tanzanian Company under Companies Ordinance (Cap. 212) and a leading Hospitality Company with its Operations in Arusha, Meatu-Simiyu and Mara Regions.

We are currently looking for short term staff to fill the below positions and be part of our Migration Camp (KOGATENDE CAMP).

1. Camp Supervisor (2),
2. Sous Chef (I),
3. Chef de Partie (2),
4. Waiter (4),
5. Housekeeper (5),
6. Driver (I),
7. Stores Assistant (I),
8. Askaris (5),
9. General Maintenance (I).

**POSITIONS REQUIREMENT**

- Certificate in Hotel Management/Hospitality/Tourism or related field from a recognized University/ College.
- 5+ years' experience working in tourism hospitality (specifically on the position applying for).
- Ability to cope and work in the bush/field.
- Ability to effectively listen, communicate with the guests.
- Ready to adhere to Company's set policies.
- Effective Time Management and attentive to details.
- Work closely with the team, flexible and eager to switch and support the team whenever required A market related salary will be rewarded for this challenging but rewarding position.

**Applicants are invited to submit their CV's/Resumes and copy of certificates to the HR Office through Reception (for hard copies) or via e-mail to Recruitment@kdtl.co.tz before 16th April 2021.**

**Email applications should have a position of the job applying for on the subject line.**

**Mwiba Holdings Limited**
**P 0 Box 2782**
**Arusha -Tanzania**
**Phone: +255 27 250 8917, Fax: +255 736 502 480**

## M'biashara kortini shtaka kughushi mkopo mil. 350/-

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA John Kyenkungu (65), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, akikabiliwa mashtaka mawili ikiwamo kughushi hati ya mkopo wa Sh. milioni 350.

Mshtakiwa huyo mkazi wa Magomeni, jijini Dar es Salaam, alisomewa mashtaka yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali Adolf Lema, alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa mashtaka mawili yote ya kughushi.

Alidai kuwa katika shtaka la kwanza tarehe na siku isiyofahamika mwaka 2014, jijini Dar es Salaam, kwa nia ya kudanganya alighushi hati ya mkopo ya mwaka huo kwa kutia saini kwamba Said Nassoro amekubali kutumia hati ya nyumba yake namba 25480 ya kiwanja namba 516 kitalu B kilichopo Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni kama dhamana ya kupata mkopo benki ya Equity ya Sh. milioni 350.

Jamhuri ilidai shtaka la pili, Agosti 23, 2014, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huku akijua na kwa nia ya kudanganya alighushi barua ya tarehe hiyo, kwa kutia saini kwamba Said Nassoro, amekubali kutumia hati yake ya nyumba kama dhamana wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa amekana mashtaka hayo.

Mahakama ilimtaka mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 100 kila mmoja na mshtakiwa awasilishe fedha taslimu Sh. milioni 75 au mali isiyohamishika yenye thamani hiyo ya fedha.

Hata hivyo, mshtakiwa ameshindwa kutimiza masharti hayo na kupelekwa mahabusu mpaka Aprili 21, mwaka huu.

# THRDC yataka marekebisho sheria vyombo vya habari

**Na Enock Charles**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umeiomba serikali kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho ya baadhi ya sheria zinazominya uhuru wa habari.

Sheria hizo ni ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015, lengo likiwa ni kuboresha uhuru wa habari nchini.

Kwa mujibu wa taarifa yake kwa umma iliyotolewa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, ilisema pamoja na malengo mazuri ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa agizo hivi karibuni la kutaka vyombo vya habari vilivyofungiwa kufunguliwa bado lipo tatizo katika sheria zilizopo kuwezesha vyombo kuwa huru kufanya kazi zake

"Tunaiomba serikali kufanyia marekebisho sheria kandamizi zinazominya uhuru wa habari nchini, pia ili kutengeneza mazingira bora ya kazi kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari tunaiomba serikali itekeleze uamuzi yaliyotolewa na Mahakama mbalimbali za kitaifa na kimataifa" ilisema sehemu ya taarifa ya Ngurumwa.

Pamoja na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015, sheria nyingine zinazolalamikiwa ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 na Kanuni za Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020 ambazo ni muhimu zirekebishwe.

Aprili 6, mwaka huu, akihutubia baada ya kuwaapisha makatibu wakuu wa wizara na wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali aliowateua, Ikulu Jijini Dar es Salaam Rais Samia aliagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyofungiwa huku kuagiza kuzingatiwa kwa sheria katika kufungia vyombo vya habari badala ya kutumika kwa ubabe.

"Nasikia kuna vyombo vya habari huko mlivifungia fungia sijui viji-TV kwa mikononi vile vifungulieni lakini wafuate sheria na miongozo ya Serikali, tusiwape mdomo wa kusema kwamba tunabinya uhuru wa vyombo vya habari lakini mhakikishe kila mliyempa ruhusa ya kuendesha chombo cha habari anafuata sheria za serikali,"alisema Rais Samia

Kauli hiyo ilipokelewa kwa furaha na waandishi wa habari pamoja na wadau wakiona ni tumaini jipya kwa uhuru wa vyombo vya habari nchini, hasa vilivyofungiwa kwa muda mrefu.

Aidha, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alitangaza kufunguliwa kwa TV zote zilizokuwa zimefungiwa huku akiwaita meza ya mazungumzo wenye magazeti yaliyofungiwa.

Mara baada ya agizo hilo, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas, alisema linahusu TV za mtandaoni pekee na siyo magazeti, jambo ambalo lilizua mjadala kwa wadau mbalimbali ambao walipinga jambo hilo.

Magazeti yaliyokifungoni ni Mwanahalisi, Mawio huku Tanzania Daima likifutiwa leseni ya chapaji, kwa makosa mbalimbali ya kitaaluma.




Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni (katikati), Mkurugenzi wa Masoko na Utafiti wa TIRA, Zakaria Muyengi (kulia) na Afisa Mtendaji Mkuu wa BritamTanzania, Raymond Komanga (kushoto) wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya uzinduzi wa huduma mpya ya Bima Kidijitali (BimikaKidijitali) itakayowezesha mteja kulipia bima kwa simu ya mkononi kupitia M-Pesa. Uzinduzi huo umefanyika jijini Dar Es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DC aiagiza polisi kuwasaka walioua mwanafunzi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Deodatus Kinawilo, ameagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watu waliofanya mauaji ya mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kahororo, Irene Revocatus.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea taarifa ya mauaji ya mwanafunzi huyo ambaye alibakwa kisha kuuawa na kutupwa kando ya Ziwa Victoria.

Kinawilo alisema serikali haiwezi kufumbia macho ukatili unaofanyika katika jamii yakiwamo mauaji ya aina hiyo.

"Polisi fanyeni msako mkali zipo taarifa mtaa huo kuna wahuni wengi sana endeleeni kufuatilia na kama wananchi wanamfahamu mtu aliyehusika namba yangu ipo wazi nitumie taarifa na itabaki kuwa siri yangu na yako," alisema Kinawilo.

Alisema matendo ya mauaji yanaondoa amani na kuweka hofu kwenye mazingira ya tukio na kuacha majonzi na simanzi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Bukoba aprili 9 , mwaka huu, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Revocatus Malimi alisema kifo cha mwanafunzi huyo kilimkuta baada ya kutumwa dukani na mama yake kwenda kununua sabuni.

Alisema baada ya taarifa hizo jeshi lilianza kufanya uchunguzi ili kuwabaini wahusika na kuwachukulia hatua. Pia, aliongeza tukio la mauaji ya aina hiyo kwa wilaya ya Bukoba ni geni na jeshi litawasaka mpaka liwakamate.

# PIRLO AMTETEA RONALDO UAMUZI WA KUTUPA JEZI




**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo hana tatizo kwa Cristiano Ronaldo kutupa jezi uwanjani baada ya kushindwa kufunga wakati Juventus wakiibuka na ushindi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, dhidi ya Genoa.

Dejan Kulusevski, Alvaro Morata na Weston McKennie kila mmoja alifunga wakati Juve wakipata ushindi wa 3-1 pale kwenye dimba la Allianz, Jumapili.

Ronaldo amefunga mabao 32 kwa 'Bianconeri' hao msimu huu, lakini juzi Jumapili alishindwa kufunga bao.

Nahodha huyo wa Ureno alivua jezi yake na kuitupa chini katika dakika ya mwisho ya mchezo huo na kocha, Pirlo hakuwa na tatizo na uamuzi huo.

Pirlo alisema: "Alikuwa anataka kufunga. Yeye ni mmoja wa mabingwa kwa sababu mara zote anataka kuacha alama, lakini haya ni mambo ya kawaida na huwa yanatokea."

Juve walikuwa kwenye presha baada ya kutawala mchezo kipindi cha kwanza na wakajikuta kwenye hatari zaidi baada ya Gianluca Scamacca kufunga bao la uongozi kipindi cha pili.

Na Pirlo alikuwa na neno huhusu hilo, kwamba Genoa walionekana kuwa mchezoni.

Aliongeza: "Haikuwa rahisi, mwishoni mwa kipindi cha kwanza tulikuwa na nafasi, lakini tulikosa umakini.



# Tuchel: Havertz ni bora kuliko Costa

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema mshambuliaji wake, Kai Havertz, hahitaji kuwa mtukutu katika goli kama Diego Costa ili aonekane bora, kwa sababu tayari ameshaonyesha hilo.

Havertz alianza katika mechi dhidi ya Crystal Palace walipoibuka na ushindi wa 4-1, akifanikiwa kutoa pasi moja ya bao na kufunga mara moja.

"Kifupi si mtu mwenye hisia sana, au kuona amekasirika," Tuchel aliwaambia waandishi wa habari baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu, Jumamosi.

"Wachezaji wengine, unahisi lazima wapambane na wengine kupata kasi.

"Yeye si mtu wa aina ya Diego Costa. Hii ni rahisi. Sitamtaka kila mara kuwa hivyo. Wakati mwingine huwezi kuchanganya na lugha yake ya mwili, haionyeshi kila kitu. Ana tabia ya utulivu sana na tunafahamu ubora wake.

"Sijui kiwango atakachofikia na haraka kiasi gani. Ninaweza tu kurudia kwamba aliondoka kwenye eneo lake alilolizoea akitokea Leverkusen kuja Ligi Kuu England.

"Hivyo anahitaji kujipa changamoto na yupo hapa na ni juu yake kuonyesha ubora wake," aliongeza Tuchel.

# PSG sasa yawatolea macho Kane, Salah

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain, inawatolea macho washambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane na nyota wa Liverpool, Mohamed Salah kama ndio warithi wa Kylian Mbappe, kwa mujibu wa Telefoot.

Majaliwa ya Mbappe pale PSG yamekuwa mjadala mkubwa kwani kuna uwezekano mkubwa wa kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

PSG wanajua kwamba, Mbappe ana nia kubwa ya kutaka kujiunga na miamba wa soka la Hispania, Real Madrid ambao wameonyesha wazi kabisa kwamba wanaisaka saini yake kwa udi na uvumba.

Na Mbappe mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kwenda kucheza kwenye klabu hiyo ambayo amekuwa shabiki wake tangu utotoni.

Na sasa PSG wameweka orodha ya wachezaji wake inaotaka kuwasajili kwa ajili ya kuziba pengo la Mbappe.

Kane na Salah ndio wanaonekana kuwa chaguo lao namba moja kwa ajili ya kutua hapo kwenye viunga vya Jiji la Paris.

Kane ameonyesha wazi kwamba, anataka kuondoka kule Spurs kwa ajili ya kusaka mataji, huku Salah naye akitajwa kutaka changamoto mpya na anataka kondoka pale Liverpool.



**HABARI MICHEZO**

# Klopp alilia mashabiki Anfield

**LONDON,** England

JURGEN Klopp amesema kufanya vibaya kwa Liverpool msimu huu katika Uwanja wa Anfield kunatokana na kukosekana kwa mashabiki wao.

Baada ya kupoteza mchezo dhidi ya Crystal Palace Aprili 17, 2017, Liverpool ilicheza mechi 68 bila kufungwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, ambapo rekodi hiyo ilivunjika baada ya kufungwa na Burnley Januari mwaka huu.

Kipigo dhidi ya Burnley kilifuatiwa na timu hiyo kupoteza mechi nyingine sita mfululizo kwenye Uwanja wa Anfield, vipigo vilivyoonekana kumshtua Klopp, aliyeibuka na sababu kuwa ni kutokana na kucheza bila ya mashabiki wao.

Hata hivyo, amesema kukosekana kwa mashabiki wao kwenye uwanja huo, hakuwezi kuwa sababu pekee ya kufanya vibaya, lakini anaamini mashabiki wa timu hiyo ambao wanachukuliwa kuwa bora kwenye uwanja wao wa nyumbani ni moja ya sababu ya wao kutopata matokeo mazuri msimu huu.

"Moja ya sababu ni kukosekana kwa mashabiki wetu, hakuna shaka na hilo," alisema akinukuliwa na BT Sport.

"Timu nyingi zina tatizo hilo. Mbali na sababu hiyo kwa nini hatushindi mechi zetu za nyumbani ni kwa sababu hatuchezi vizuri.

"Kuna baadhi ya mechi za nyumbani tulizopoteza ambazo nafikiri hata bila mashabiki tulipaswa kushinda kwa uhakika kabisa, lakini hatukushinda.

"Sasa tuna mlolongo wa kupoteza mechi za nyumbani. Mechi sita mfululizo. Hizi ni mechi nyingi.







# AC MILAN, VAZQUEZ WAANZA MAZUNGUMZO YA MKATABA

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imeripotiwa kuwa tayari imeanza kufanya mazungumzo ya kumsajili winga wa Real Madrid, Lucas Vazquez kama mchezaji huru, kwa mujibu wa Calciomercato.

Milan inakumbana na upinzani wa kuiwania saini hiyo kutoka kwa klabu za Inter Milan, Bayern Munich na Manchester United.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Mkurugenzi wa Ufundi wa Milan, Paolo Maldini, tayari ameshawasiliana na uwakilishi wa mchezaji huyo, licha ya kipaumbele cha nyota huyo wa Hispania kuwa ni kuendelea kusalia Real Madrid.

Uwakilishi wa Vazquez umedai kuhitaji mkataba mpya wa miaka minne, wenye thamani ya euro milioni tano kwa mwaka.

Lakini taarifa zaidi kutoka nchini Hispania zimesema kuwa si Real Madrid wenyewe au Milan ambao wapo tayari kwa masharti hayo.

Milan wao kwa upande wao wanaweza kumpa mkataba wa mwaka wa euro milioni nne, ikiwa ni kiwango kikubwa zaidi wanachoweza kumlipa mchezaji ukiachana na Zlatan Ibrahimovic na Gigio Donnarumma.

# *Inter yakaribia ubingwa Serie A*

**MILAN,** Italia

BAO la mlinzi wa pembeni, Matteo Darmian, liliiwezesha Inter Milan kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Cagliari Jumapili, wakati kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte kikikaribia kulibeba taji la Serie A kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 11.

Wanaojikongoja Cagliari walionekana kuwa wagumu kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la San Siro, huku golikipa Guglielmo Vicario, ambao huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza, akiokoa hatari nyingi na kuwafanya vinara hao kuendelea kuwa kwenye nafasi nzuri.


Licha ya wageni hao kujaribu kulinda sana lango lao, lakini Darmian aliwatungua dakika ya 77 na kuwa bao lake la pili kwenye ligi, huku Inter wakipata ushindi wao wa tisa mfululizo.

Inter sasa inaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 11 dhidi ya AC Milan waliopo nafasi ya pili huku mechi nane zikiwa zimebaki na Cagliari wamebaki nafasi ya 18.

"Hizi mechi ni za kupambana sana, tunatakiwa kuendelea kucheza kwa uhodari kwa mechi zote zilizobaki," alisema Conte akiiambia DAZN mara baada ya mchezo huo.



# DOND ZA SOKA
## MAGA A ULAYA




# CAVANI AZIDI KUMTOA JASHO SOLSKJAER UTD

**●●● Anajua hisia zangu, najua hisia zake, bado hajafikia uamuzi ila naamini anaweza...**

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer bado ana matumaini ya kumshawishi Edinson Cavani kubaki Manchester United baada ya straika huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye ushindi dhidi ya Tottenham.

**'Mashetani Wekundu' hao walitoka nyuma kwa bao moja na kupata ushindi wa 3-1 pale London Kaskazini Jumapili na kupunguza pengo la pointi hadi 11 dhidi ya vinara Manchester City, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.**

Cavani alishuhudia bao lake kipindi cha kwanza likikataliwa na VAR, huku Scott McTominay akilimwa kadi ya njano kwa kumshika usoni Son Heung-min.

Son akaiweka mbele Spurs, kabla ya Fred kusawazisha na Cavani kuongeza la pili kwa krosi ya Mason Greenwood na baadaye akafunga bao la tatu.

Cavani alisaini mkataba wa mwaka mmoja tu na United baada ya kuondoka pale Paris Saint-Germain, lakini straika huyo mzoefu hakuwa na mwanzo mzuri sana nchini England, huku virusi vya corona vikimfanya kucheza mechi chache na pia alifungiwa mechi tatu kwa kauli ya kibaguzi.

Baba mzazi wa mchezaji huyo awali alionyesha kwamba, Cavani anataka kurudi Amerika Kusini msimu ujao, akihusishwa na mpango wa kujiunga na Boca Juniors, lakini Solskjaer hajakata tamaa ya kuongeza mkataba wa mwaka mmoja zaidi kwa mchezaji huyo.

"Edi alionyesha kwa nini ni namba tisa," alisema Solskjaer akiiambia Sky Sports. "Tulikuwa na mikutano michache na vijana. Kwa wakati huu tunahitaji kuwatumia vizuri zaidi.

"Anajua hisia zangu; najua hisia zake. Bado hajafikia uamuzi. Naelewa umekuwa mwaka mgumu kwa kila mtu, lakini kwa mtu mpya ambaye hazungumzi Kiingereza, hana utamaduni wa Uingereza, kuona watu wakiwa na marafiki zao na yeye hana ni jambo gumu kwake.

"Nimefunga vidole vyangu, naamini anaweza kubaki baada ya msimu huu, tumekuwa na bahati naye nzuri."

Cavani sasa amefunga mabao saba kwenye ligi msimu huu, matano kwa kichwa - akipitwa na straika wa Everton, Dominic Calvert-Lewin aliyefunga sita kwa kichwa.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO AMTAKA KANE

KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino, amewasiliana na mshambuliaji nyota wa Tottenham na timu ya Taifa ya England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, kuhusu uwezekano wa kuhamia Ufaransa. ***(Telefoot on Twitter)***

### KLOPP ATAJWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich itajaribu kumsajili kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp mwishoni mwa msimu huu huku Hansi Flick akienda kuitumikia timu ya Taifa ya Ujerumani. ***(90mins)***

### ARSENAL KUIPIKU WEST HAM

ARSENAL inapanga kuipiku West Ham kwenye mbio za kumsajili kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 28 kipindi kinachokuja cha majira ya joto. ***(Star)***

### LIVERPOOL, BARCA NA PEDRI

LIVERPOOL wanatakiwa kumsajili haraka kiungo wa Barcelona, Pedri mwenye umri wa miaka 18, kabla hajasaini mkataba mpya utakaoongeza fedha nyingi kwenye kipengele cha kumuuza. ***(Star)***

### PSG WAJITOSA KWA SALAH

KLABU ya Paris St-Germain imewasiliana na wawakilishi wa Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 28, kuhusu kumsajili kutoka Liverpool wakati wa kipindi cha majira ya joto, nyota huyo wa Misri. ***(Telefoot)***

### MOURINHO AMWANIA FELLAINI

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, anapanga kumsajili kiungo wa Ubelgiji, Marouane Fellaini mwenye umri wa miaka 33, ambaye pia alikuwa chini yake kule Manchester United. Fellaini kwa sasa yupo na klabu ya Shandong Luneng ya China tangu Februari 2019.

### SOUMARE AKARIBIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City ipo mbele ya Manchester United katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa klabu ya Lille, Boubakary Soumare mwenye umri wa miaka 22. ***(Star)***

### TORRES AGOMBEWA ULAYA

MANCHESTER United wanamtaka "kwa udi na uvumba" beki wa klabu ya Villarreal na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anawaniwa na vigogo wengine wa soka barani Ulaya, Bayern Munich na Real Madrid. ***(AS, via Team Talk)***

### DYBALA HAKIELEWEKI JUVE

MAZUNGUMZO baina ya Juventus na mshambuliaji wake, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, ambaye anahusishwa na mipango ya kutaka kuhamia Manchester United, bado haijakamilika kutokana na hali ya kifedha ya klabu hiyo ya Turin, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa ufundi, Fabio Paratici. ***(Sky Italia, via Goal)***

## HABARI MICHEZO

## NAMUNGO YAPOTEA CAF, RAJA CASABLANCA YA KWANZA KUFUZU

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC, wakipoteza matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali, washindani wao kutoka Kundi D, Raja Casablanca ya Morocco, wamekuwa wa kwanza kufuzu hatua hiyo baada ya kufikisha pointi 12 kutoka katika michezo minne.

**Namungo ambayo ipo Kundi D pamoja na Raja Casablanca, Nkana FC ya Zambia na Pyramids FC ya Misri, juzi ikiwa ugenini nchini Zambia ilikubali kipigo cha pili mfululizo cha bao 1-0 kutoka kwa Wazambia hao baada ya mechi ya awali jijini Dar es Salaam kupoteza kwa idadi hiyo.**

Matokeo hayo yanaifanya Namungo sasa kupoteza mechi zake zote nne za mwanzo kwenye michuano hiyo baada ya kufungua dimba kwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Raja Casablanca ugenini kabla ya kurejea nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kuangukia pua kwa mabao 2-0 dhidi ya Pyramids.

Kwa namna msimamo wa kundi lao ulivyo ambapo Raja Casablanca juzi ilifuzu hatua ya robo fainali baada ya kuibuka na ushindi ugenini wa mabao 3-0 dhidi ya Pyramids, ni wazi Namungo sasa haina nafasi tena ya kufuzu robo fainali kutokana na kuburuza mkia bila pointi hadi sasa huku Wamisri hao na Nkana wakichuana kusaka nafasi ya pili ili kufuzu wakati huu kila moja ikiwa na pointi sita.

Juzi ilikuwa siku ya Wakongomani baada ya kuzipa timu zao ushindi, ambapo kwenye mechi ya Raja Casablanca mabao yao dhidi ya Pyramids yalifungwa na Fabrice Ngoma na Ben Malango huku la tatu likizamishwa nyavuni na nyota wa Morocco, Soufiane Rahimi.

Kwa upande wa mechi ya Nkana pia bao lake lilifungwa na Mkongomani Freddy Tshimenga dakika ya 71 na kuipa ushindi huo dhidi ya Namungo.

Akizungumzia matokeo hayo, Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco amesema kinachoigharimu timu hiyo ni kukosa uzoefu kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

"Tayari tumerejea nchini, upungufu ambayo tunauona tutaufanyia kazi ili kupata matokeo kwenye mechi zetu zijazo," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Namungo FC, Kindamba Namlia, alisema licha ya kupoteza na kuonekana kutokufanya vizuri, lakini kuna hatua kubwa wamepiga kwa kujifunza mambo mengi kupitia michuano hiyo wanayoshiriki kwa mara ya kwanza.

**UZINDUZI...**




Mwenyekiti wa Matawi na Wanachama wa Klabu Yanga, Saad Kimjii (kulia), akizindua Tawi la Kivule la klabu hiyo, Kivule, jijini Ilala, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Wa pili kushoto ni mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Edibily Lunyamila na wa tatu kulia ni Mwenyekiti tawi hilo, Abubakar Kindagule. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *KMC yafunguka inapozishika Simba, Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema huwa haizikamii timu kubwa kama mtazamo wa wengi, ikiwamo baadhi ya wachambuzi wa soka nchini, badala yake huwa wanajipanga kucheza kutokana na timu wanayocheza nayo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, ndiye aliyetoa kauli hiyo baada ya kauli za baadhi ya wadau wa soka kuwa KMC imekuwa ikizikamia timu kubwa hasa za Simba na Yanga.

Hii inakuja baada ya Jumamosi iliyopita kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga, Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Nimepigiwa simu nyingi sana baada ya mechi eti tunaambiwa mbona mnakamia sana mechi zetu Yanga? Nasikiliza hata vipindi vya michezo wanasema KMC huwa tunakamia mechi kubwa za Simba na Yanga. Ukweli ni kwamba sisi hatukamii, ila tunacheza mechi kutokana na mpinzani tunaekwenda kucheza naye.

"Haiwezekani unakwenda kucheza na Simba au Yanga halafu unakwenda kucheza kitoto kama unakwenda kucheza na timu zingine za kawaida, maafa yanaweza kukukuta, ndiyo maana makocha wetu huwa wanaongeza dozi ya mazoezi na mbinu," alisema.

Aliwataka mashabiki kutodhani kuwa Simba na Yanga ndiyo wana haki ya kushinda tu, kwani hata timu zingine ikiwamo KMC zina wachezaji bora ambao wanaweza kuzichezea timu hizo na wakang'ara.

"Si uliona mwenyewe, Yanga walitamani mpira uishe, lile ndiyo 'pira spana', 'pira mapato', tunawapongeza vijana wetu kwa kupambana na mashabiki wetu pia kwa kutushangilia, mechi tumeimaliza na sasa tunajiandaa na mechi ya tarehe 16 dhidi ya Gwambina FC, " alisema Christina.

KMC inakamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 36 kwa mechi 25 ilizocheza huku Yanga ikiongoza kileleni kwa alama 51 baada ya kushuka dimbani mara 24.

## Mapinduzi kurejea dimbani Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoonekana uwanjani kwa muda mrefu, nyota wa Yanga, Balama Mapinduzi, anatarajiwa kurejea rasmi dimbani Julai mwaka huu akiwa fiti, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema majeraha ya Balama yalikuwa makubwa sana kwa sababu alivunjika na yupo katika uangalizi mkubwa.

Alisema nyota huyo amekuwa na program tofauti na kuna muda anatakiwa kutembea kwa kutumia fimbo maalum na mara nyingi anatakiwa kuacha na kuanza kutembea bila ya msaada wa kiti chochote.

"Kwa mujibu wa madaktari wanaomtibu, wamesema hadi Julai mwaka huu atakuwa fiti na kuanza kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiweka fiti kabla ya kurejea uwanjani kucheza mechi za ushindani.

"Mbali na Balama hakuna majeruhi mwingine, tunaendelea vizuri na maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Biashara United kuhakikisha tunafanya vizuri na kupata pointi tatu muhimu," alisema Mwambusi.

Alisema hakuna mechi rahisi katika mzunguko wa lala salama na kila timu inayokutana na Yanga inahitaji kupata pointi ili kujinasua katika nafasi iliyopo hususan katika kuepuka kushuka daraja.

## Ligi Zanzibar zapisha Mwezi wa Ramadhani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL) imesema Ligi Daraja la Kwanza Kanda na Ligi Kuu Zanzibar zitaenda mapumziko ili kupisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao jana ulitarajiwa kuanza leo Aprili 13, kwa kutegemea kuandama kwa mwezi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamo Mwenyekiti wa bodi hiyo, Sheha Mohammed, alisema ligi hiyo itarejea mara baada ya kukamilika Mwezi wa Ramadhani na funga ya sita ili kumalizia michezo sita kwa kila timu iliyobaki Ligi Kuu na ile ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja huku Kanda ya Pemba ikiwa ndio kwanza umechezwa mzunguko mmoja.

Alisema kuchelewa kumalizika mapema kwa ligi hizo msimu huu kumetokana na kusimama hususan katika vipindi vya misiba ya viongozi wa kitaifa.

# Michezo

Jumanne Aprili 13, 2021

Nipashe




Cavani azidi kumtoa jasho Solskjaer Utd UKURASA 22

KIKOSI KAZI...



Kikosi kazi cha Simba ambacho kesho kitaikaribisha Mtibwa Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa moja usiku, kikiwa mazoezini. **PICHA: SIMBA**

# Ubingwa Yanga SC ni ngumu - Jembe Ulaya

## ●●● Awatetea viongozi huku akilia na wachezaji kuwaangusha na viwango vyao vikishuka kwa...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Yanga kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC Jumamosi, usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuzua simanzi na malalamiko kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo, mchezaji wa zamani wa klabu hiyo, Bakari Malima 'Jembe Ulaya', ameibuka na kusema lawama zote zielekee kwa wachezaji kwa kutojituma huku akiondoa matumaini ya ubingwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Jembe Ulaya, beki wa zamani wa timu hiyo yenye maskani yake Jangwani, alisema anachokiona ni kwamba wachezaji wanawaangusha viongozi wao kwani kila simu zinavyozidi kusonga mbele viwango vyao vinaonekana kushuka.

"Hakuna kitu kizuri kama kuambiana ukweli. Ni kwamba hapa wachezaji ndio wanawaangusha viongozi wao. Viongozi wanajitahidi sana, wanawaweka kwenye kambi nzuri, wanakula vizuri, wanalala pazuri, kila kitu wanapata, " alisema beki huyo wa kati wa zamani.

**Malima alisema wao kama wachezaji wa zamani wamekuwa wakiwasiliana vizuri na viongozi wa Klabu ya Yanga, Kamati ya Ufundi, pamoja na benchi la Ufundi kuwapa ushauri na wamekuwa wakipata ushirikiano mzuri na kila kitu kinakwenda sawa, lakini mwisho ndani ya uwanja wachezaji ndio wanaotakiwa kupambana kukamilisha vitu vyote ambavyo wamefanya na kushauriana.**

Kuhusu kutetea ubingwa, Jembe Ulaya alisema pamoja na kwamba bado uko wazi, lakini kwa Yanga ni ngumu kutwaa ubingwa msimu huu.

"Tuseme tu ukweli. pamoja na kwamba mpaka sasa ubingwa uko wazi kwa timu yoyote, lakini ninavyoona kwa Yanga sasa ni ngumu. Wanachotakiwa kufanya ni kupambana ili kupata zile nafasi nne za juu ambazo zinaweza kuwafanya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao kama Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho," alisema.

Pamoja na sare hiyo, Yanga bado inaongoza kwa pointi 51, lakini kwa sasa inafuatiliwa kwa karibu na Azam FC yenye pointi 47, huku Simba ambayo kesho inacheza dhidi ya Mtibwa Sugar ina pointi 46, ikiwa nyuma michezo minne dhidi ya kinara huyo.

Yanga itashuka tena katika Uwanja wa Mkapa Jumamosi kuikaribisha Biashara United ambayo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 40 zilizotokana na mechi 24.

# Mtibwa hofu kwa Simba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitarajiwa kwenda kuivaa Simba kesho kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Mtibwa Sugar imeonekana kama kuingiwa na hofu kutokana na ubora wa wapinzani wao kwa sasa.

Akizungumza akiwa jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru, alisema wako kwenye matayarisho ya mechi hiyo, lakini itakuwa ngumu na wana kazi kubwa ya kufanya kutokana na ubora mkubwa walionao wapinzani wao kwa sasa.

"Tunakwenda kucheza na moja kati ya timu bora Afrika kwa sasa, hakika ni mechi ngumu na tuna kazi ngumu ya kufanya, kama unavyojua tulipoteza mechi hivi karibuni kwa kufunga mabao 2-0 dhidi ya Azam. Bado hatujaondoka Dar es Salaam tunaisubiri mechi hiyo," alisema.

Kuhusu tathmini ya mchezo wenyewe, Kifaru alionekana kutarajia bahati zaidi kuliko uwezo wa timu yao. "Lolote linaweza kutokea, hata wao Simba pamoja na uzuri wao wote wana upungufu wao, tunaweza tukayatumia na kupata ushindi."

Hata hivyo, alisema timu itacheza mechi hiyo bila kuwapo Kocha Mkuu Thierry Hitimana ambaye aliondoka kutokana na kukorofishana na baadhi ya wasaidizi wake kwenye benchi la ufundi.

"Kocha Hitimana hadi sasa hajarejea na timu itaongozwa na Vicent Barnabas," alisema Kifaru.

Mtibwa inakamata nafasi ya 15 kwa pointi 24, huku ikiwa imecheza mechi 23 mpaka sasa wakati Simba iliyoshuka dimbani mara 20 ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 46.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >